# USWUWL AS-SUNNAH

# ‘Misingi Ya Sunnah’

## Imaam Ahmad

**(Imekusanywa Katika Mfumo Wa Maswali Na Majibu)**

**Imefasiriwa Na:**
**Naaswir Haamid**

Maswali na majibu yafuatayo yameratibiwa ili kuujaribu ufahamu wa msomaji katika nukta kuu za *'Aqiydah* (Itikadi na *Iymaan*) na M*anhaj* (Mfumo/Njia). Nukta nyingi katika hizi zilizojaribiwa zimechukuliwa kutoka kitabu cha *Uswuwl As-Sunnah* ('Misingi Ya Sunnah'), kilichoandikwa na Mwanachuoni mkuu Imaam Ahmad bin Hanbal (Rahimahu Allaah). Ingawa ni vyema kutumia kitabu hiki, maswali yanaweza kujibiwa bila ya kutumia kitabu hichi.

Faida za ziada zimepatikana kutoka vitabu vyengine vya *'Aqiydah* na M*anhaj*. Hivyo, msomaji asije kuvunjika moyo iwapo hatopata kitu cha kujibu kupitia kitabu cha *Uswuwl As-Sunnah*. Nukta inawezekana imechukuliwa kutoka kitabu na vyanzo vingine ambavyo vitatajwa kwa sehemu hizo, na mara kadhaa kutafsiriwa kwa Kiswahili chini ya jibu.

Maswali yamegawanywa katika mpango wa somo la wiki tisa.

Maswali na majibu tofauti ya kuchagua yametayarishwa na Ummu Zaynab 'Aaliyah bint Ihsaanullaah (Rahimaha Allaah).

★Tafadhali zingatia kwamba chaguzi zaidi ya moja inawezekana ikawa sahihi★

**Mwongozo wa Mpango wa Kusoma**

| WIKI | TAREHE | NUKTA | MADA |
|---|---|---|---|
| 1 | | 1-6 | *Manhaj* sahihi<br>Uzushi |
| 2 | | 7-16 | Nafasi ya *Sunnah Qadar*<br>(Kutizamia) |
| 3 | | 17-21 | *Ru-yah*<br>*Kalaam* (Dhana ya ufasaha wa kusema) |
| 4 | | 22-27 | Qur-aan haijaumbwa<br>Kumuona Allaah |
| 5 | | 28-36 | Mada ya Siku ya Mwisho |
| 6 | | 37-46 | *Iymaa.*<br>Maswahaabah |
| 7 | | 47-59 | Viongozi wa Waislamu |
| 8 | | 60-68 | Nani anayekwenda Peponi na Motoni<br>Adhabu Zilizoelezwa<br>Kuwazungumzia vibaya Maswahaabah |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 9 | | 69-75 | Unafiki<br>Kujifunga na maandiko<br>Pepo na Moto zipo tayari<br>Kuwaswalia watu wa Q*iblah* |

# Wiki 1 Nukta 1-6

Swali: 1. Nani aliyeandika *Uswuwl As-Sunnah* ('Misingi Ya Sunnah')?

1. Abuu Muhammad Ahmad bin Muhammah bin Hanbal
2. Abuu 'Abdir-Rahmaan Ahmad bin Hanbal
3. Abuu Abdillaah Ahmad bin Muhammad bin Hanbal

**Jibu: 3. Abuu Abdillaah Ahmad bin Muhammad bin Hanbal**

Swali: 2. Ni kipindi gani ambacho kwa kukisia Imaam Ahmad aliishi?

1. Miaka 100 baada ya *Hijrah*
2. Miaka 200 baada ya *Hijrah*
3. Miaka 400 baada ya *Hijrah*

**Jibu: 2. Alizaliwa mwaka 164 H na kufariki katika mwaka 241 H.**

Swali: 3. Nini maana ya neno '*Sunnah*' kwa minajili ya jina la kitabu *'Uswuwl as-Sunnah'*?

1. Sayansi ya *Hadiyth*
2. Kanuni za *'Aqiydah* na M*anhaj*
3. Utofauti baina ya njia ya *Salaf* na zile za madhehebu potofu
4. Njia ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam)

**Jibu: 2, 3 na 4. Kutoka katika hadidu za chini (footnotes) za 'Misingi Ya Sunnah' (cha Fawwaaz Ahmad Zumarliy): "*Sunnah* kwa hapa inamaanisha kanuni na misingi ya usahihi wa *'Aqiydah* ya Kiislamu (Itikadi na *Iymaan*) na M*anhaj* (mfumo), kwani *Salaf* hutumia neno hili la 'Aqiydah na Manhaj**

**– kama inavyoonekana katika vitabu na maandiko yao, kwa mfano ... [anataja 11 miongoni mwao]. Neno *Sunnah* limetumiwa katika maandiko haya kutofautisha baina ya yale Maswali ya *'Aqiydah* na M*anhaj* ambayo *Salaf* walikuwa dhidi ya mambo hayo yaliyozuliwa na madhehebu yaliyokengeuka na potofu."**

Swali: 4. Jaza pengo katika tamko la Imaam Ayyuwb As-Sakhtiyaaniy (aliyefariki mwaka 131 H):

"Kutoka katika mafanikio ya kijana au asiyekuwa Muarabu ni kwamba Allaah Anamuongoa katika..."

1. Mwanachuoni wa ki-Sunnah
2. *Hadiyth* sahihi za Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam)
3. Njia ya Imaam Ahmad bin Hanbal

**Jibu: 1. Nukuu hii ipo katika hadidu za chini (footnotes) za 'Misingi Ya Sunnah'.**

## Maswali Ya Nukta 1-2

Swali: 5. Jaza pengo ndani ya maneno ya ufunguzi ya Imaam Ahmad: "Misingi mikuu ya Sunnah kwetu sisi ni: kukamatana na yale ambayo..."

1. Mjumbe wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) alikuwa akiyakubali.
2. Maswahaabah wa Mjumbe wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) walikuwa wakiyakubali.
3. Wanachuoni wa *Hadiyth* walikuwa wakiyakubali.




**Jibu: 2. Namna utakavyoendelea kusoma sehemu hii ndivyo utakavyopata jibu ni kwa nini jibu halikuwa ni namba 1.**

Swali: 6. Ni nani *Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah*?

1. Mtu yeyote anayetumia jina hilo kwa manufaa yake.
2. Wale ambao wanaoshikamana vyema kwa yale ambayo Maswaahabah wakiyakubali.
3. Kundi kubwa la Waislamu.

**Jibu: 2. Nukuu ya chini imechukuliwa kutoka fatwaislam.com ikinukuu Al-*Majmuu' fiy tarjumah Hamaad Al-Answaariy*, juzuu ya pili, ukurasa wa 762-763.**

**Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano ambayo Shaykh Hammaad ameweka wazi ni nani watu *Sunnah*:**

**Muulizaji: Ni nani *Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah*?**

**Shaykh: Ni wale ambao wameshikamana vyema kwa yale ambayo Maswahaabah wakiyakubali.**

**Muulizaji: Je, *Salafiy* ni miongoni mwa *Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah*?**

**Shaykh: Ndio; *As-salafiyyah* ni *Sunnah* na *Jamaa'ah*, hii ni kwa sababu**

**maana ya *Salafiyyah* ni kushikamana vyema kwa yale ambayo *Salaf* wema wakiyakubali hapo kabla.**

**Muulizaji: Ee Shaykh; Je, makundi ya *Ikhwaan* (*Al-Muslimuwn*) na *At-Tabliygh* – Je, wao wanatokana na *Ahlus-Sunnah*?**

**Shaykh: Kila mtu aliyekuwa na fikra ambayo ni kinyume na *Ahlus-Sunnah* basi hao hawatokani nao (Ahlus-Sunnah), hivyo makundi ya *Ikhwaan* (*Al-Muslimuwn*) na *At-Tabliygh* hayatokani na *Ahlus-Sunnah*, kwa sababu wapo juu ya fikra ambazo ni kinyume nao (Salafiy).**

Swali: 7. Ni ipi sifa ya dhehebu miongoni mwa madhehebu 73 ambayo yameokolewa kutokana na Moto, kama yalivyotajwa ndani ya *Hadiyth*?

1. "Kwa yale ambayo mimi na Maswahaabah zangu tumeshikamana nayo leo."
2. "Wale ambao wanaoifuata Qur-aan na *Sunnah* yangu."
3. "Wale ambao wana *Iymaan* na *Taqwaa* ndani ya mikutano yao na Mola wao."

**Jibu: 1. Angalizo kwamba kuna misamiati mingine ya Hadiyth, lakini kitu kimoja kwa wakati!**

Swali: 8. Ni madhehebu mangapi kati ya hayo 73 yalidai kufuata Qur-aan na *Sunnah*?

1. Hakuna hata moja.
2. Dhehebu lililookolewa.
3. Yote hayo.

**Jibu: 3. Shaykh Al-Albaaniy amesema: "Hivyo alama inayotofautisha dhehebu lililookolewa si tu kama makundi mengine ndani ya enzi zetu zinavyodai. Alama inayotofautisha dhehebu hili si tu kwamba inajihusisha lenyewe kwa kutenda kwa mujibu wa Kitabu na *Sunnah*. Kwani haiwezekani kwa kila mtu miongoni ma Waislamu – hata kama watakuwa nje ya madhehebu yaliyookolewa – haiwezekani kwa kila mtu kutoka miongoni mwa madhehebu haya, ya zamani na mapya, kujitoa kutokana na kufuata Kitabu na *Sunnah*. Hii ni kwa sababu kama watafanya hivyo, basi watakuwa wameashiria kuachana na Uislamu. Kutokana na hivyo,**

**makundi yote ya Kiislamu na madhehebu yote ya Kiislamu ni madhehebu ya Mjumbe (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) yaliyotajwa au yaliyooneshwa ndani ya *Hadiyth* iliyopita. Madhehebu haya yote yanashiriki katika neno moja. Hakika, ni kujihusisha kwa Kitabu na *Sunnah*." Kitabu cha Misingi ya Mfumo wa Salafiy, tarjuma ya Kiingereza, ukurasa 19.**

Swali: 9. Je, makundi [Waislamu] ya leo ni miongoni mwa madhehebu 73 ambayo yanaelekea katika uharibifu?

1. Ndio. Yote hayo, isipokuwa *Ahlus Sunnah wal-Jamaa'ah*.
2. Baadhi yao, na mengine sio. Haturuhusiki kutoa maoni juu ya lolote miongoni mwao kama ni sahihi au sio sahihi.
3. Hapana. Inamaanisha kwa yale ambayo yamehusika na kutoamini (kufr).

**Jibu: 1. Shaykh Swaalih al-Fawzaan amesema katika kujibu suala linalofanana na hilo: "Kila mtu anayepinga *Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah* kutoka miongoni mwa wale wanaojihusisha wenyewe na Uislamu katika njia ya *Da'wah*, au *'Aqiydah*, au kitu chochote miongoni mwa nguzo za *Iymaan*, basi hayo yanaingia miongoni mwa madhehebu sabini na moja na onyo (la Moto) linawafaa wao. Atahukumiwa na kuadhibiwa kwa namna alivyopinga." Imechukuliwa kutoka fatwaislam.com, ikinukuu kitabu cha *Al-Ajwibah al-Mufiydah*.**

Swali: 10. Je, kuna madhehebu 73 tu miongoni mwa Waislamu.

1. Ndio.
2. Hapana.
3. Tamko lililo sahihi zaidi ni kwamba kuna madhehebu 73 ambayo ni msingi wa hayo madhehebu, kutoka hapo kuna matawi katika madhehebu mengi.

**Jibu: 3. Ndio sahihi zaidi. Shaykh Swaalih al-Fawzaan amesema katika kujibu suala mfano wa hilo: "Hii si katika njia ya kukataza, kwa hakika madhehebu haya yapo mengi (kwa idadi). Na iwapo utasoma na kuchunguza vitabu vilivyoandikwa kuhusu madhehebu, utakuta kwamba yapo kwa idadi kubwa. Hata hivyo – na Allaah Anajua zaidi – madhehebu haya sabini na tatu ni msingi wa madhehebu, kisha baada ya hapo**

**yanatoka matawi ya madhehebu mengi. Na wala hakuna kundi la leo lenye upinzani wa watu wa *Sunnah*, isipokuwa yanatokana na madhehebu haya na matawi yanayotokana nayo.”**

## Maswali Ya Nukta 3

Swali: 11. Je, ni ipi tafsiri ya Imaam ash-Shaatwibiy kuhusu B*id'ah* (jambo jipya lililozuliwa/uzushi)

1. "Jambo jipya lililozuliwa ndani ya Diyn, katika kuiga *Shari'ah* ambapo ukaribu na Allaah unatafutwa, bila ya kutegemezwa kwa ushahidi sahihi – si katika misingi yake wala namna ya utendaji wake."
2. "Jambo jipya lililozuliwa ndani ya Diyn, mfanyaji ambaye ana niyyah ya kutenda maovu kwa matendo yake, na jambo ambalo halina msingi ndani ya Qur-aan wala *Sunnah*."
3. "Jambo jipya lililozuliwa ndani ya Diyn, bila ya ushahidi sahihi, lakini jambo ambalo halimtoi mtu nje ya Uislamu."

**Jibu: 1. Fikiria kuihifadhi maana hii ya B*id'ah*.**

Swali: 12. Je, yepi yafuatayo ni uzushi ndani ya Diyn?

1. Kusherehekea kuzaliwa kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam)
2. Kusema maneno ya kumkumbuka Allaah ndani kwa mkusanyiko
3. Kuswali rak'ah ya tano katika Swalah ya Adhuhuri
4. Kuhusisha mchana na usiku wa katikati ya mwezi wa Shaa'baan (Niswfush-Sha'abaan) kwa kuswali na kufunga
5. Kukana yaliyokadiriwa kabla (Qadar)

**Jibu: 1, 2, 3, 4, na 5. Zote hizi zimetajwa na Shaykh Swaalih al-Fawzaan ndani ya Kitabu cha Tawhiyd.**

Swali: 13. Je, kuna kitu kinachoitwa [Bid´ah] uzushi mzuri ndani ya mas-alah ya Diyn?

1. Ndio, na mambo haya yanalipwa.
2. Hapana, kila uzushi ni upotofu.
3. Kuna tofauti inayokubalika miongoni mwa wanachuoni kuhusiana na hili.

**Jibu: 2. Kuna Hadiyth, ambayo ndani yake Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema: "… na kila uzushi ni upotofu na kila upotofu unapelekea kuingia Motoni." Hadiyth sahihi iliyosimuliwa na An-Nasaaiy 1/224. Ibn 'Umar (amefariki mwaka 84H) amesema: "Kila uzushi ni upotofu, hata kama watu watauona kuwa ni kitu kizuri." [Imesimuliwa na Abu Shaamah (namba 39)]**

Swali: 14. Je, ni mambo gani yanayochukiwa mno na Allaah kwa mujibu wa Ibn 'Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhu)?

1. Dhambi zote kubwa
2. Maovu makuu saba yanayoangamiza yaliyotajwa ndani ya Hadiyth
3. Bid´ah [Uzushi]

**Jibu: 3. Ibn Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhuma) amesema: "Hakika, mambo yanayochukiwa mno na Allaah, Mtukufu, ni uzushi." [Imetajwa ndani ya hadidu za chini kama zilivyosimuliwa na Al-Bayhaqiy]**

Swali: 15. Je, yepi kati ya yafuatayo ni zaidi kuliko uzushi?

1. Shirk (kumshirikisha Allaah na kitu ambacho ni makhsusi haki Yake)
2. Maovu makuu saba yanayoangamiza
3. Maovu makuu
4. Kufr (kutoamini)

**Jibu: 1 na 4, lakini jibu hili linahitaji maelezo zaidi.**

**Ama kwa 1, basi Allaah Amesema ndani ya Qur-aan: "Hakika Allaah Hasamehe kushirikishwa; na Husamehe yasiyokuwa haya kwa Amtakaye. Na anayemshirikisha Allaah bila shaka amebuni dhambi kubwa." [An-Nisaa]**

**Ama kwa 2 na 3, Imaam ash-Shaafi'iy (amefariki mwaka 204H) amesema: "Kwamba mtu atakutana na Allaah kwa kila ovu isipokuwa Shirk, ni bora kuliko kukutana Naye katika imani za uzushi." [Imesimuliwa na al-Bayhaqiy ndani ya *al-I'tiqaad* (uk.158)]. Sufyaan ath-Thawriy amesema: "Uzushi unapendwa zaidi na Ibliys (Shaytwaan) kuliko madhambi. Hii ni kwa sababu madhambi yanayoweza kuombewa *tawbah* lakini kwa uzushi hayaombewi *tawbah* [kwa urahisi]." [Kutoka *Majmuu´ al-Fataawaa* 11/472].**

**Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema: "Hakika, Allaah amezuia tawbah kwa kila mtu wa uzushi." [*As-Silsilah asw-Swahiyhah* namba 1620. Marejeoyamechukuliwa kutoka katika hadidu za chini za Majibu yenye Manufaa kwa Shaykh al-Fawzaan, ukurasa 31].**

**Ama kwa 4, basi kuna aina mbili za *bid'ah*. (1) Ile ambayo inafikia kiwango cha kufr. (2) Ile ambayo haifikii kiwango cha kufr, hivyo kwamba mtu ambaye anaifanya anabakia kuwa ni Muislamu. Rejeo: *Qawlul-Mufiyd* (Risaalah yenye Manufaa... cha Shaykh al-Waswaabiy).**

Swali: 16. Kama tutamuona mtu anafanya uzushi, Je, tumtambue moja kwa moja kama ni mzushi?

1. Hapana
2. Ndio

**Jibu: 1. Abuu Daawuwd as-Sijistaaniy (amefariki mwaka 275 H) amesema: "Nilimwambia Abuu 'Abdillaah Ahmad bin Hanbal, 'Iwapo nitamuona mtu kutoka *Ahlus-Sunnah* amekaa na mtu kutoka watu wa uzushi, Je, niache kuzungumza naye?' Akasema: 'Hapana. Kwanza umueleze kwamba yule uliyemuona naye ni mtu wa uzushi. Akiacha kuzungumza na mzushi, basi endelea kuzungumza naye, iwapo si hivyo, basi mchukulie kuwa ni kama yeye (mzushi)." Ibn Masu'uwd (Radhiya Allaahu 'anhu) amesema: "Mtu ni kama rafiki yake." [Imesimuliwa na Ibn Abiy Ya'laa. Rejeo ni ndani ya 'Misingi Ya Sunnah', ukurasa 169].**

## Maswali Ya Nukta 4-6

Swali: 17. Kwa mujibu wa Imaam Ahmad, ni kutokana na 'Misingi Ya Sunnah' kuacha kuketi pamoja na watu wa matamanio (yaani wazushi) (Nukta 6). Haya ni maoni ya nani?

1. Maoni tofauti ya Imaam Ahmad
2. Wanachuoni walio wengi
3. Baadhi ya wanachuoni, lakini si wengi kati yao
4. Wanachuoni wote wa *Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah*

**Jibu: 4. *Qaadhi* Abuu Ya'laa (amefariki 333H) amesema: "Kuna makubaliano (*Ijmaa'*) miongoni mwa *Swahaabah* na *Taabi'iyn* (waliowafuata Maswahaabah) kuhusiana na kutojumuika na kuwapiga pande wazushi." [Angalia ukurasa 164 wa 'Misingi Ya Sunnah'].**

Swali: 18. Je, tunaweza kusikiliza mawaidha/mihadhara ya wazushi?

1. Hapana.
2. Ndio, kila wanapozungumza kuhusiana na mas-alah yatakayoathiri mioyo yetu na kututengezea *Iymaan*.
3. Ndio, kila wanapokua na 'ilmu zaidi yetu.
4. Ndio, kila tunapokuwa katika sehemu iliyo mbali na watu wa *Sunnah*.

**Jibu: 1. Ibn Qudaamah (amefariki mwaka 620H) amesema: "*Salaf* walikuwa wakizuia kukaa pamoja na wazushi, kuangalia vitabu vyao na kusikiliza maneno yao." [*Al-Adaabush-Shari'ah*. Nukuu imetolewa kutoka 'Misingi Ya Sunnah' uk.165].**

Swali: 19. Tumheshimu vipi mmoja kati ya *Salaf* pale tunapomuona amekaa pamoja na mzushi?

1. Tumpige pande, bila ya kuzungumza naye.
2. Tumshauri. Kama akiendelea kwa kosa hili, basi amiliana naye kama unavyoamiliana na mzushi.

3. Lipuuzie hilo, na endelea kuamiliana naye kama ilivyokuwa kabla.

**Jibu: 2. Angalia nukuu ya Imaam Ahmad iliyonukuliwa hapo juu katika jibu la Sswali: 16.**

Swali: 20. Kwa nini inazuiliwa kukaa pamoja na wazushi?

1. Tunaweza kutumbukia katika upotofu wao, na kuchanganyikiwa na vitu ambavyo tulikuwa tukivielewa.
2. Tunakhofia kwamba watatufanyia istihzai.
3. Tunakhofia kwamba tutaondokana na hifadhi ya Allaah.
4. Ni alama ya unaafiq.
5. Wazushi wameacha Uislamu.
6. Wanawatoa watu katika ukweli.
7. Laana inaweza kutuangukia.

**Jibu: 1, 3, 4, 6 na 7.**

**Ama kwa 1: Abuu Qulaabah amesema: "Usikae pamoja nao na wala usichanganyike nao, kwani sijisikii salama kwamba watakuzamisha katika upotofu wao na kukuchanganya kwa yale mengi uliyokuwa ukiyafahamu." [*Sharh Uswuwlul-I'tiqaad* cha al-Laalikaa'iy (namba 244)].**

**Ama kwa 3: Sufyaan ath-Thawriy (amefariki mwaka 161H) amesema: "Yeyote anayesikiliza wazushi ameacha hifadhi ya Allaah na ameshikana na wazushi." [Imesimuliwa na Abu Nu'aym ndani ya *al-Hilyah* (7/26) na Ibn Battah (namba 444)].**

**Ama kwa 4: (266).... al-Fudhwayl amesema: "Allaah ana Malaaikah wanaotafuta mikusanyiko ya dhikr – kwa hivyo angalia ni mikusanyiko gani unayokaa – isijekuwa ni pamoja na wazushi kwani Allaah hatowaangalia, na alama za Unaafiq ni kwamba mtu anasimama na anakaa pamoja na wazushi." [*Sharh Uswuwlul-I'tiqaad* cha al-Laalikaa'iy (namba 265)].**

**Ama kwa 6: Al-Fudhwayl bin 'Iyaadhw amesema: "Iwapo mtu amekuja kwa mtu kushauriana naye na kumuelekeza kwa mzushi, basi ameufanyia *khiyaanah* Uislamu. Kuwa na tahadhari kwenda kwa mzushi kwani wanawatoa watu kutoka kwenye ukweli." [*Sharh Uswuwlul-I'tiqaad* cha al-Laalikaa'iy (namba 261)].**

**Ama kwa 7: Al-Fudhwayl amesema: "Usikae pamoja na mzushi kwani ninakhofia kwamba laana itawaangukia juu yenu." [*Sharh Uswuwlul-I'tiqaad* cha al-Laalikaa'iy (namba 267)].**

Swali: 21. Je, sisi, Waislamu wa kawaida, tuwakabili viongozi wa uzushi na kuwakanya?

1. Ndio
2. Hapana

**Jibu: 2. Al-Hasan al-Baswriy (amefariki mwaka 110H) amesema: "Usikae pamoja na wazushi na watu wa matamanio, wala usijadiliane nao, wala usiwasikilize." [Imesimuliwa na ad-Daarimiy ndani ya *Sunan* yake (1/121)].**

Swali: 22. Ni hukumu gani kwa makundi ya Kiislamu (zaidi ya Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah)?

1. Wamepotoka.
2. Si waumini.
3. Iwapo watapingana na *Jamaa'ah* ya *Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah*, basi wamepingana na M*anhaj* ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam).

**Jibu: 1 na 3. Shaykh Swaalih al-Fawzaan amesema: "Kila mtu anayepingana na *Jamaa'ah* ya *Ahlus-Sunnah* basi amepotoka. Hatuna isipokuwa *Jamaa'ah* moja, nayo ni *Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah*. Chochote kitakachopingana na hichi, basi hicho kimepingana na Manhaj (mfumo) wa Mjumbe (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam)." [Imechukuliwa kutoka fatwaislam.com, ikinukuu kutoka kitabu cha *Al-Ajwibah al-Mufiydah*].**

## Wiki 2 Nukta 7-16

### Maswali Ya Nukta 7-9

Swali: 1. Jibrily alikuwa akishuka na ipi miongoni mwa hizi chini?

1. Qur-aan pekee
2. Qur-aan na *Sunnah*
3. Qur-aan na sehemu za *Sunnah*.

**Jibu: 2. Hasaan bin Atwiyyah (amefariki mwaka 120H) amesema: "Jibriyl alikuwa akishuka kwa Mjumbe wa Allaah akiwa na *Sunnah* kama alivyokuwa akishuka akiwa na Qur-aan." [Rudia hadidu za chini za 'Misingi Ya Sunnah', tarjama ya Kiingereza ukurasa 12].**

Swali: 2. Jaza pengo ndani ya tamko la Yahyaa bin Kathiyr (amefariki mwaka 129 H):

"Sunnah ni ___________________ Kitabu cha Allaah."

1. Kubwa kuliko
2. Wazi zaidi
3. Yenye ufafanuzi juu ya

**Jibu: 3. Rejeo: Sunan ad-Daarimiy. Angalia hadidu za chini za 'Misingi Ya Sunnah'.**

Swali: 3. Ni alama gani unaiona pale mtu anapowachukia watu wa simulizi (wa Hadiyth)?

1. Yeye ni mtu wa uzushi
2. Yeye ni mtu asiyeamini

3. Yeye ni mtu wa *Ahlus-Sunnah* lakini mwenye *Iymaan* dhaifu.

---

**Jibu: 1. Imaam Abu Haatim ar-Raaziy (amefariki mwaka 264AH) amesema: "Alama ya mtu wa uzushi ni kwamba anawavamia wale waliokamatana na masimulizi (Hadiyth za Mtume)." [*Ahlus-Sunnah wal I'tiqaadud-Diyn*. Nukuu imechukuliwa kutoka 'Misingi Ya Sunnah', tarjama ya Kiingereza, ukurasa 161].**

---

## Maswali Ya Nukta 10-12

Swali: 4. Ni neno lipi linaeleza vizuri zaidi maana ya *hawaa* ndani ya maelezo haya?

1. Upepo
2. Hawa (mke wa Aadam)
3. mjuzi
4. matamanio

---

**Jibu: 4. Wingi wake ni *ahwaa* (matamanio). Ibnul Qayyim amesema: "Mara nyingi *al-hawaa* inatumika kuwaelezea makatazo ya kugandana na utashi." ['Kupinga al-Hawaa', ukurasa 16].**

---

Swali: 5. Ni kipi kinyume cha *hawaa*?

1. *Taqwaa*
2. Ukweli
3. Kile ambacho Allaah amekishusha kwa Mjumbe wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam)

---

**Jibu: 3. Ibnul Qayyim amesema: "Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) ameifanya *hawaa* ni kinyume cha Yale Aliyoyashusha kwa Mjumbe Wake. Ameifanya kuifuata kuwa ni moja kwa moja yenye kupingana na mwenendo wa Mjumbe Wake, na Ameigawa katika makundi mawili: wafuasi wa Wahyi na wafuasi wa *hawaa*. Na hii inaonekana katika sehemu nyingi za Qur-aan, kama ndani ya tamko Lake: "Na kama hawakukujibu, basi jua ya kuwa wanajifuatia tu matamanio yao." [Al-Qaswas: 50] ['Kupinga al-Hawaa', ukurasa 30].**

---

Swali: 6. Ni kwa mara ngapi ndani ya Qur-aan yule ambaye anayefuata matamanio yake ametajwa kuwa na wadhifa sawa na yule anayeabudu sanamu?

1. Moja
2. Mbili

3. Tatu

**Jibu: 2. Ibnul Qayyim amesema: "Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala) Amemfanya yule mwenye kufuata *hawaa* kuwa na wadhifa sawa na yule mwenye kuabudia sanamu. Yeye, Mtukufu, Amesema ndani ya sehemu mbili katika Kitabu Chake:** "Je, Umemuona yule aliyefanya matamanio yake, (kile anachokipenda), kuwa Mungu wake?" **[Al-Furqaan: 43 na Al-Jaathiyah: 23]. Al-Hasan Al-Baswriy (amefariki mwaka 110H) ameshereheshea: "Huyo ni mnafiq; hakuna chochote anachotamani isipokuwa anakifuata tu." Pia amesema: "Mnafiq ni mtumwa wa *hawaa* zake: hakuna chochote anachotamani isipokuwa anakitenda." [Kupinga al-Hawaa, ukurasa 33].**

Swali: 7. Ni mtu gani kati ya wafuatao wametaja yote a) kufuata na b) kutozua pamoja ndani ya nukuu moja?

1. Abuu Bakr (Radhiya Allaahu 'anhu)
2. Ibn Mas'uwd (Radhiya Allaahu 'anhu)
3. Shurayh al-Qaadhiy (amefariki mwaka 80 H)
4. Imaam Ahmad

**Jibu: Wote hao.**

**Abuu Bakr (Radhiya Allaahu 'anhu) amesema: "Hakika, mimi ni mfuasi, na wala si mzushi." [Imesimuliwa na Ibn Qudaamah. Imechukuliwa kutoka 'Misingi Ya Sunnah' hadidu za chini, ukurasa 9].**

**Ibn Mas'uwd (Radhiya Allaahu 'anhu) amesema: "Hakika, sisi tunafuata na wala hatuanzishi na tunafuata na wala hatuzui." [Imesimuliwa na al-Laalikaaiy 1/86. Imechukuliwa kutoka 'Misingi Ya Sunnah' hadidu za chini ukurasa 9]. Pia amesema: "Fuata wala usizue, kwani wewe umepewa yale ambayo yanakutosha, na kila uzushi ni upotofu." [Imesimuliwa na Abu Khaythamah. Imechukuliwa kutoka hadidu za chini za 'Maelezo ya Iymaan' cha Imaam al-Barbahaariy, ukurasa 26].**

**Shurayh al-Qaadhiy (amefariki mwaka 80H) amesema: "Hakika, *Sunnah* imeizidi Q*iyaas* yako (hoja za kimantiki) hivyo fuata na wala usizue." [Imesimuliwa na ad-Daarimiy. Imechukuliwa kutoka 'Misingi Ya Sunnah', hadidu za chini, ukurasa 12].**

**Imaam Ahmad amesema: "Isipokuwa hiyo (Sunnah) [ni mjumuiko wa] kufuata [na kujitegemea juu] yake na kukana hawaa (matamanio)." ['Misingi Ya Sunnah', ukurasa 12].**

## Maswali Ya Nukta 13

Swali: 8. Mjumbe (Swalla Allaahu ʻalayhi wa aalihi wa sallam) amesemaje kuhusiana na mtu anayeipa mgongo *Sunnah* yake?

1. Hao ni wapotofu
2. Hao hawatofanikiwa
3. Hao hawatokani naye
4. Hao ni watu wasioamini

**Jibu: 3: Yeye Mjumbe (Swalla Allaahu ʻalayhi wa aalihi wa sallam) amesema: "Yeyote anayeikimbia *Sunnah* yangu hatokani na mimi." [Al-Bukhaariy na Muslim].**

## Maswali Ya Nukta 14-16

Swali: 19. Ni matamko gani kati ya haya ni kweli kuhusiana na *Iymaan* ya *Qadar*?

1. Ni nguzo (rukn) ya Uislamu
2. Ni tawi la Uislamu
3. Ni nguzo ya *Iymaan*.
4. Ni tawi la *Iymaan*.

**Jibu: 3. Ushahidi wa hili ni *Hadiyth* ya Jibriyl.**

Swali: 10. Ni Maswahaabah gani ambao ni baba na mtoto walisimulia *Hadiyth* ya *Jibriyl*?

1. Jaabir bin ʻAbdillaah kutoka kwa baba yake ʻAbdullaah
2. An-Nuʼmaan bin Bashiyr kutoka kwa baba yake Bashiyr
3. ʻAbdullaah bin ʻUmar kutoka kwa baba yake ʻUmar

4. Hasan bin ʻAliy kutoka kwa baba yake ʻAliy

**Jibu: 3. Nayo ni *Hadiyth* ya mwanzo iliyoletwa na Imaam Muslim ndani ya Swahiyh yake.**

Swali: 11. Kwa mujibu wa msimulizi wa Hadiyth, Yahya bin Ya'mar, ni nani alikuwa mtu wa mwanzo kukana Qadar ndani ya mji wa Basra?

1. Ma'bad al-Juhaniy
2. Jahm bin Safwaan
3. Ja'd bin Dirham

**Jibu: 1.**

Swali: 12. Ni nani alikuwa msimulizi wa Yahya bin Ya'mar akitamani kukutana pale alipokwenda Makkah akiwa pamoja na mwenzake, kwa muono wa kujua kuhusu Q*adar*?

1. Mtume (Swalla Allaahu ʻalayhi wa aalihi wa sallam)
2. *Swahaabah* wa Mjumbe (Swalla Allaahu ʻalayhi wa aalihi wa sallam)
3. Maalik ibn Anas

**Jibu: 2. Hii imetajwa na wasimulizi wa Hadiyth. Alifurahi kumuona Ibn 'Umar (Radhiya Allaahu 'anhuma)**

Swali: 13. Ni lini uzushi wa kukana Q*adar* ulijitokeza kwa mara ya mwanzo?

1. Wakati wa maisha ya Mtume (Swalla Allaahu ʻalayhi wa aalihi wa sallam)
2. Wakati wa maisha ya baadhi ya Maswahaabah
3. Wakati wa maisha ya *Taabi'iyn* (wale waliofuata baada tu ya Maswahaabah)

**Jibu: 2. Angalia hadidu za chini za 'Misingi Ya Sunnah', na 'Kitabu cha Tawhiyd' cha Shaykh Swaalih al-Fawzaan**

Swali: 14. Ni maneno gani yaliyotajwa na msimulizi yanayoonesha kwamba kuna watu wa uzushi wanaofanya matendo mengi ya ki-´Ibaadah?

1. "Wamejitokeza baadhi ya watu ndani ya ardhi zetu ambao wanasoma Qur-aan na kutafuta ʻilmu (ya Diyn)..."
2. "Kuna watu ambao kwa kuswali kwao kutakufanya uone *Swalah* yako kutokuwa na maana."
3. "Kuna alama katika vipaji vya nyuso zao kutokana na kusujudu kwao."

**Jibu: 1. Alikuwa akizungumzia kuhusiana na wale wanaokana Qadar.**

Swali: 15. Shaykh al-´Uthaymiyn amesema: "*Iymaan* ya *al-Qadar* haikamiliki hadi pale mtu anaposhuhudia vitu vinne." Ni upi mpangilio sahihi?

1. elimu – maandiko – utashi – uumbaji
2. uumbaji – utashi –maandiko – elimu
3. elimu – utashi – maandiko - uumbaji

**Jibu: 1. Rejeo: Ufafanuzi wa Kuhusu *Iymaan* Yenye Kutosheleza (*Lum´atul I´itiqaad*, tarjama imefanywa na Shaykh al-ʻUthaymiyn) ukurasa 100.**

Swali: 16. Ni wapi tutapata ushahidi kwamba Allaah Ameumba matendo ya watumwa wake?

1. Ndani ya Qur-aan
2. Ndani ya *Sunnah* lakini si Qur-aan
3. Ndani ya matamko ya Maswahaabah, lakini si kwenye Qur-aan wala kwenye Sunnah

**Jibu: 1.** "Hali Allaah Ndiye Aliyekuumbeni nyinyi na mnavyovifanya." **[Asw-Swaafaat: 96]**

Swali: 17. Watu wa *Qadariyyah* ni dhehebu linalopinga Q*adar*. Ni matamko gani kati ya haya ni kweli kuhusiana na *Iymaan* ya *Qadariyyah*?

1. *Qadariyyah* wanasema kwamba matokeo hutokea katika Uumbaji wake Allaah ambavyo Allaah hakutaka kutokezea – Ametakasika Allaah kwa yale wanayosema.
2. Wanahusisha kutokuwa na ukamilifu kwa Allaah.
3. Wanaenda mbali hadi kuhakikisha utashi wa mja.
4. Wanashindwa kuthibitisha utashi wa Allaah.
5. Wanaamini kuwepo waumbaji wengi, kila mtu akiumba matendo yake mwenyewe.
6. Wao ni *Majuws* (waabudu moto) wa Ummah huu.

---

**Jibu: Zote ni sahihi. Maneno yafuatayo yote yamechukuliwa kutoka kwenye kitabu cha Shaykh Swaalih al-Fawzaan, 'Mtazamo [kwa ufupi] wa Madhehebu Potofu'.**

**Dhehebu la mwanzo kwa upotofu liliokuja lilikuwa ni dhehebu la *Qadariyyah*. Hii ilikuwa ni mwisho wa kipindi cha Maswahaabah (Radhiya Allaahu 'anhum)**

***Qadariyyah* wanakana Q*adar* na kusema: "Chochote kinachotokezea duniani hakitokani na Q*adar* na Q*adhwaa* ya Allaah, isipokuwa ni jambo linalotokana kutokana na matendo ya mja (kiumbe), bila ya hukumu ya kabla kutoka kwa Allaah." Kwa hivyo wanakana nguzo ya mwisho ya *iymaan* ambayo ni: '*Iymaan* ya Allaah, Malaaikah Wake, Vitabu Vyake, Mitume Wake, Siku ya Mwisho na *Iymaan* katika Q*adar*, vizuri na vibaya vyake, vyote vishakadiriwa na Allaah.'**

**Wamepewa jina la '*Qadariyyah*' na pia 'Majuws' (wanaoabudu moto kwa Ummah huu) kutokana na kwamba wanadai kila mtu anaumba matendo yake na hakuna hata moja linalotokezea kutokana na amri ya Allaah. Hivyo wanathibitisha waumbaji pamoja na Allaah kama walivyo *Majuws* wanaosema: 'Ulimwengu una waumbaji wawili, nuru na giza. Nuru imeumba mazuri na Giza imeumba mabaya.' Hata hivyo, *Qadariyyah* wamekwenda mbali zaidi ya *Majuws* kwa kuthibitisha waumbaji tofauti kwa kusema kwao: 'Kila mtu anaumba matendo yake mwenyewe.'**

---

Swali: 18. Ni kundi gani ambalo linalokwenda kinyume mno dhidi ya *Qadariyyah* katika suala hili?

1. Salafiy
2. Mu'tazilah
3. Jabariyyah

---

**Jibu: 3. Ifuatayo ni muendelezo wa moja kwa moja wa nukuu sawa iliyotumika katika suala lililopita:**

**Na wapinzani wao ni *Jabariyyah*, wanaosema kwamba kila mja analazimika kutenda matendo yake na wala hana khiyari yoyote, isipokuwa tu yeye ni kama ubawa unaopepea katika upepo bila ya khiyari. Hivyo wamekuja kujulikana kama ni *Jabariyyah* na wamekwenda mbali mno katika kuthibitisha Q*adar* kama walivyotolewa khiyari waja katika jambo lolote.**

**Kundi la kwanza (*Qadariyyah*) ni kinyume nao moja kwa moja; wanathibitisha khiyari kwa mtu lakini wakaenda mbali mno katika hilo hadi kwamba kusema: 'Mtu anaumba matendo yake mwenyewe bila ya Allaah', Allaah yupo mbali kabisa kwa yale wanayoyasema. Na miongoni mwao ni Mu'tazilah na wale wanaofuata njia zao.**

**Hivyo, kuna madhehebu mawili yaliyopotoka katika Q*adar*:**
**i. Wale waliokwenda mbali mno katika kukana**
**ii. Wale waliokwenda mbali mno katika kukubali**

---

Swali: 19. Je, kuna madhehebu mangapi ya *Qadariyyah*:

1. Mawili
2. Saba
3. Idadi kubwa zaidi

---

**Jibu: 3. Ifuatayo ni muendelezo wa moja kwa moja wa nukuu sawa iliyotumika katika suala lililopita:**

***Qadariyyah* wamegawanyika katika makundi tofauti na Allaah tu ndiye anayejua idadi zao. Pale mtu anapoacha ukweli basi anazurura ovyo katika upotofu, kila kundi inazua wenyewe madhehebu yake na hivyo kutawanyika kutoka kundi lililopita. Hii ndio asili ya watu wapotofu, kila wakati wakitofautiana, wakitawanyika na kuvumbua fikra na dhana**

**mgongano kwao wenyewe. Ama kwa *Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah*, kutofautiana na kuchanganyikiwa havijitokezi miongoni mwao kwa sababu wanashikana katika ukweli uliotokana na Allaah na *Sunnah* ya Mjumbe wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) na wapo juu ya M*anhaj*.**

## Maswali Kuhusu *Ru-yah*

Swali: 1. Ni wapi Allaah Anaweza kuonekana, na kwa nani?

1. Hapa duniani kwa Mitume wawili tu
2. Katika Siku ya Hukumu kwa watu wote, ikiwemo wasioamini
3. Katika viwanja maalumu vya Siku ya Hukumu kwa waumini
4. Peponi kwa waumini

---

**Jibu: 3 na 4.**

**Shaykh al-'Uthaymiyn amesema katika sherhe ya *Iymaan* Yenye Kutosheleza ukurasa 95:**

**"*Salaf* wote kwa pamoja wamekubaliana kwamba waumini watamuona Allaah, sio kama wasioamini, wakitumia ushahidi [Aayah ya 15 ya Suuratul-Mutwaffifiyn]. Watamuona Allaah katika sehemu ya mwisho ya kisimamo cha Siku ya Hesabu na baada ya kuingia Peponi, kama Allaah Atakavyopenda." Pia amesema, ndani ya kitabu hicho: "Kumuona Allaah ndani ya maisha ya dunia hii haiwezekani, kutokana na kigezo cha tamko la Allaah kwa Muusa pale alipoomba kumuona Yeye:** "Hutaniona (ndani ya maisha haya)." **[Al-A'raaf: 143]**

---

Swali: 2. Ni matamko gani kati ya haya ni kweli?

1. *Ru-yah* ni neno la Allaah.
2. *Ru-yah* ni sifa ya Allaah.
3. *Ru-yah* ni taarifa za Allaah, lakini sio sifa Yake.

---

**Jibu: 2. Shaykh Swaalih al-Fawzaan amesema ndani ya Ufafanuzi wa Al-'Aqiydah at-Twahaawiyyah (mwisho wa nukta ya 59) kuhusiana na *ru-yah*: "... kwa sababu ni kama mfano wa sifa zilizobakia za Allaah, Mtukufu na Muweza..."**

---

Swali: 3. Kwa hili jibu likiwemo kichwani, ni utaratibu gani sahihi juu ya maandiko ya Qur-aan na *Sunnah* kuhusiana na *ru-yah*?

1. Tunathibitisha kuwa maandiko kuhusiana nayo katika maana ya maandiko na maneno.
2. Tutafute maana nyengine kwa maandiko hayo pale yanapokuwa na kitu ambacho ni kigumu kukifahamu.
3. Tunaweza kutafuta ufafanuzi wa maandiko hadi tuone (ufafanuzi) mmoja ambao unakubaliana na mantiki zetu.
4. Tunazipita kama zilivyokuja kwetu.

---

**Jibu: 1 na 4.**

**Ibn Qudaamah amesema: "Kuhusiana na Hadiyth:** 'Hakika Allaah hushuka katika mbingu ya chini kabisa' **na** 'Hakika Allaah Ataonekana Siku ya Hukumu' **na kile kinachofanana na Hadiyth hizi, Imaam Abuu 'Abdillaah Ahmad bin Hanbal amesema: 'Tunaamini katika hayo, na tunashuhudia kwa ukweli wake bila ya kuuliza vipi, na bila ya kutoa maana [isiyo sahihi]. Na wala hatukani chochote kutokana nazo, na tunatambua kwamba chochote alichokileta nacho Mtume basi ni Sahihi, na hatukani chochote kinachotokana na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam)." Rejeo: Lum'atul-I'tiqaad cha Ibn Qudaamah al-Maqdisiy. Tafsiri ya nukta hii imechukliwa kutoka katika seti ya darsa za kusikiliza (audio), ambazo sasa zinapatikana katika tovuti ya www.ittibaa.com**

**Abu Bakr al-Marwaziy (amefariki mwaka 294 AH) amesema: "Nilimuuliza Ahmad ibn Hanbal kuhusiana na Hadiyth ambazo Jahmiyyah wamezikataa kuhusiana na sifa, waumini kuweza kumuona Mola wao Siku ya Hukumu, Utukufu wa Allaah, na '*Arsh* yake. Hivyo Abuu 'Abdillaah (Imaam Ahmad) akatamka kuwa zote kuwa ni sahihi na kusema: 'Wanachuoni wamezipokea kwa kuzikubali. Tunazirithisha kwa vizazi vitakavyokuja kwetu sisi." Angalia Hadidu za chini za 'Misingi Ya Sunnah', ukurasa 16.**

---

Swali: 4. Ni kwa namna ipi Allaah Ataonekana?

1. Hatuulizi kuhusu 'vipi' Sifa zake ndizo hizo!!!
2. Ataonekana wazi na waumini kwa macho yao.
3. Anaweza tu kuonekana kwa mioyo ya waumini.
4. Ataonekana bila ya utaratibu maalumu.

**Jibu: 1 na 2.**

**Ama kwa 1, hatuulizi kuhusu 'vipi' kwa sifa za Allaah (angalia nukuu za hapo juu).**

**Ama kwa 2, ushahidi wa hili unapatikana katika Hadiyth nyingi ambazo zimetufikia katika hadhi ya *mutawaatir* (zimesimuliwa na wasimulizi tofauti katika kila awamu), kama alivyotamka yeye (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) pale yeye na Maswahaabah zake walipokuwa wakiangalia mwezi katika usiku wa mwezi uliojaa (full moon):**

'Hakika mtamuona Mola wenu kama vile mlivyouona mwezi huu, hamtaingizwa katika matatizo hadi kumuona Yeye.' **[Hadiyth imesimuliwa na Al-Bukhaariy (553) na Muslim].**

Swali: 5. Kwa mnasaba wa makosa ambayo watu wanayaingia kuhusiana na sifa za Allaah:

Linganisha kosa liliopo upande wa kushoto pamoja na maana yake katika upande wa kulia.

| | |
|---|---|
| Takyiyf | Kukana sifa kwa pamoja |
| Tamthiyl | Kuuliza ni vipi Sifa ipo |
| Ta'twiyl | Kupotosha Sifa kwa kutoa maana isiyo sahihi |
| Tahriyf | Kufananisha Sifa ya Allaa kwa Sifa ya Uumbaji |

**Jibu:**

| | | |
|---|---|---|
| **Takyiyf** | **–** | **Kuuliza ni vipi Sifa ipo** |
| **Tamthiyl** | **–** | **Kufananisha Sifa ya Allaah kwa Sifa ya Uumbaji** |
| **Ta'twiyl** | **–** | **Kukana Sifa kwa pamoja** |
| **Tahriyf** | **–** | **Kupotosha Sifa kwa kutoa maana isiyo sahihi** |

**Shaykh-ul-Islaam ibn Taymiyyah amesema ndani ya 'al-'Aqiydah al-Waasitwiyyah'**

**"Na katika I*ymaan* kwa Allaah ni: Kuwa na I*ymaan* katika lolote ambalo amelitangaza Mwenyewe ndani ya Kitabu Chake na ndani ya lolote ambalo Mtume Wake amelieleza, bila ya kutumbukia katika *tahriyf* au *ta'twiyl* na bila ya kutumbukia katika *takyiyf* au *tamthiyl*.'**

Swali: 6. Ni zipi kati yake zinatambulikana kuwa na misemo ya kipotofu kuhusiana na maana ya *ru-yah*?

1. Katika kuona malipo ya Allaah (lakini sio kumuona Allaah)
2. Katika kuona 'ilmu na uhakika (lakini sio kumuona Allaah)
3. Allaah Ataonekana, lakini kwa maelekezo
4. Allaah Hataonekana

**Jibu: zote hizo ni sahihi. Angalia Ufafanuzi wa Iymaan Yenye Kutosheleza cha Shaykh al-'Uthaymiyn ukurasa 95, na Ufafanuzi wa Twahaawiyyah cha Shaykh al-Fawzaan, sasa vinapatikana katika njia ya kusikiliza kwenye** www.ittibaa.com

S7. Ni matamko gani ya kipotofu katika suala lililopita yatambulike kuwa ni kalaam (usemaji fasaha wa 'ilmu ya tabia na sifa za Allaah na Diyn).

**Jibu: Zote hizo. *Kalaam* ni usemaji fasaha wa hotuba inayohusisha mjadala wa kihoja kuhusiana na Diyn, lakini sio juu ya kanuni zozote za Kiislamu.**

S8. Sema ni nani amesema: "Yeyote anayeitafuta *Diyn* kupitia *kalaam* atapotoka."

**Jibu: Imaam Maalik. Rejeo: Iymaan ya Maimamu Wanne, ukurasa 40.**

S9. Sema ni nani aliyesema: "Hukumu yangu kuhusiana na watu wa *kalaam* ni kwamba wapigwe kwa majani ya mtende na viatu na wapangwe mstari miongoni mwa jamaa na makabila huku ikitangaziwa: 'Haya ndio malipo ya yule anayeiacha Kitabu na *Sunnah* na akaelekea katika *kalaam*."

**Jibu: Imaam ash-Shaafi'iy. Sharh Twahaawiyyah cha Ibn Abiy al-'Izz ukurasa 75 (Rejeo imechukuliwa kutoka hadidu za chini ya 'Misingi Ya Sunnah', ukurasa 17).**

Swali: 10. Ni wanachuoni gani wanaotambua kuruhusika kutumia *kalaam*?

1. Ibn Siriyn
2. Az-Zuhriy
3. Hakuna hata mmoja kati yao, kwa makubaliano

**Jibu: 3. Ibn 'Abdil-Barr amesema: "Watu wa *Fiqh* na A*thar* (wasimulizi) katika mitaa na miji yao tofuati walikuwa wakikubaliana kwa pamoja kwamba watu wa *kalaam* (si watu, isipokuwa) ni watu wa uzushi na upotofu. Na wala hawatambuliki, kwa wote hapo juu, kuwa ni miongoni mwa hadhi za wanachuoni (wa ukweli)." Imesimuliwa na Ibn Qudaamah ndani ya Burhaan fiy Bayaanil Qur-aan. Rejeo imechukuliwa kutoka hadidu za chini za 'Misingi Ya Sunnah', ukurasa 17.**

Yafuatayo ni Maswali yaliyochukuliwa kutoka katika ufafanuzi wa al-Aqiydah at-Twahaawiyyah cha Shaykh Swaalih al-Fawzaan kinachopatikana katika www.islamthestudyguides.wordpress.com

Yafuatayo ni baadhi ya Maswali kuhusiana na ru-yah:

**MASWALI YANAYOHUSIANA NA NUKTA 58**

**7) Katika maelezo ya Imaam (Rahimahu Allaah):**

***Na ru-yah kwa watu wa Peponi ni Kweli...***

- ***ru-yah ina maana gani?***

***Ru-yah*** **ina maana ya 'kuona' na inahusisha kwa waumini kuweza kumuona Mola wao (Subhaanahu wa Ta'ala) katika Siku ya Hukumu.**

**8) Je, hii *ru-yah* inatokea katika njia ya kihalisia au ni kifikra tu? Je, ni upi ushahidi wa hili?**

**Waumini watamuona Mola wao kihalisia, kwa macho yao wenyewe, kama wanavyouona mwezi katika usiku wa mwezi uliojaa.**

**Ushahidi wa hili unapatikana ndani ya *Ahaadiyth* ambazo zimetufikia sisi kwa njia ya *mutawaatir*, kama zile alizoeleza Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) pale alipokuwa yeye na Maswahaabah zake wakiangalia mwezi katika usiku wa mwezi uliojaa:**

'Hakika mtamuona Mola wenu kama mlivyouona mwezi huu, hamtatatizika katika kumuona Yeye.' **[Hadiyth imesimuliwa na Al-Bukhaariy (554) na Muslim].**

**9) Ni vipi Shaykh (Hafidhahu Allaah) anavyoeleza kuhusiana na maneno ya Imaam:**

← *Ru-yah (kwa watu wa Peponi) ni Haqq (kweli)?*

**Ni H*aqq* kwa maana ya kwamba imeelezwa ndani ya Kitabu, *Sunnah*, na Makubaliano ya *Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah* tokea enzi za vizazi vya mwanzo hadi vya mwisho wake. Hakuna hata mmoja anayekataa jambo hili isipokuwa kwa wazushi na watu wa madhehebu yaliyopotoka.**

**10)** **<u>Ni nyuso za nani zimeelezwa ndani ya Aayah ya Suuratul-Qiyaamah [75: 22-23]?</u>**

Baadhi ya nyuso Siku hiyo zitakuwa *Naadhirah* (zinangara).
*Naadhwirah ilaa* (zikimuangalia) Mola wao. **[Suuratul-Qiyaamah (75) Aayah za 22-23].**

**Hii inamaanisha kwa nyuso za waumini.**

**15)** **<u>Ni ushahidi gani miwili kutoka thibati za Qur-aan ambazo Shaykh anaziweka bayana katika kuonesha kwamba waumini watauona Uso wa Mola wao Siku ya Hesabu?</u>**

Kwa wale waliofanya mema [malipo yao] ni *al-husnaa* na *az-ziyaadah* (kitu kizuri kwa ziada ya hili). **[Suurat Yuunus (10) aayah ya 26].**

**Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) ameeleza kuwa *husnaa* ndani ya Aayah hii ina maana ya Pepo na akaeleza *ziyaadah* kumaanisha kumuona kwa macho yake mwenyewe, mtu kuuona Uso wa Allaah (Hadiyth sahih iliyosimuliwa na Muslim – 181).**

Hapo watapata yote wanayotaka – na Tuna *al-maziyd* (jambo zaidi) kwao.
**[Suuratul-Qaaf (50) Aayah ya 35]**

***Maziyd* ndani ya Aayah hii ina maana ya kuangalia Uso wa Allaah.**

**16)** **<u>Ni kwa namna gani Shaykh ametumia Aayah ya Suuratul-Mataffifiyn (83 : 15) kuthibitisha kwamba waumini watamuona Mola wao Siku ya Hesabu?</u>**

Hapana! Hakika, katika Siku hiyo, hao watazuiwa kumuona Mola wao.
**[Suuratul-Mutwaffifiyn (83) Aayah 15].**

**Neno 'kuzuiwa' hapa linamaanisha kwamba hawatomuona Allaah, Mtukufu, kwa sababu hawakumuamini ndani ya dunia hii. Hii kwa hakika ni utengefu na adhabu kubwa – na hifadhi ya Allaah inapatikana kwa hapa. Hivyo hili inamaanisha kwamba wale waliokuwa wakimuamini Allaah (ingawa kiuhakika hawajapatapo kumuona hapa duniani) hawatazuiwa kumuona Allaah katika Siku ya Hesabu.**

**17)** **<u>Imaam Ibn al-Qayyim (Rahimahu Allaah) amesemaje kuhusiana na Ahaadiyth ambazo zinathibitisha kwamba waumini watamuona Allaah Siku ya Hesabu?</u>**

**Amesema kwamba zipo nyingi hadi kufikia nafasi ya *mutawaatir*.**

**18) <u>Ama kwa wale ambao wamerehemewa kwa kunufaika na nafasi ya kumuona Allaah Siku ya Hesabu, Je, hili litakuwa ni jambo gumu kwao? Kuna ushahidi gani kwa hili?</u>**

**Hapana, haitakuwa ni kazi ngumu kwao, kama inavyooneshwa katika *Hadiyth*:**

Hakika mtamuona Mola wenu Siku ya Hesabu kama ambavyo mlivyouona mwezi huu katika usiku wa mwezi uliojaa, na kama ambavyo mlivyoliona jua likingara kwa uwazi, pale ambapo hakuna mawingu (kulizuia). Hamtaingizwa matatizoni kwa kumuona Yeye – (au katika simulizi nyengine) hamtakimbia na kujumuika pamoja katika kumuona Yeye. **[Hadiyth imesimuliwa na Imaam Al-Bukhaariyh (554, 806 na 7434) na Muslim].**

**19) <u>Je, wanasemaje Jahmiyyah na Mu'tazilah kuhusiana na *ru-yah*?</u>**

**Makundi haya mawili mapotofu yanakana kumuona Allaah Siku ya Hesabu.**

**20) <u>Ni ipi dhana isiyo sahihi ambayo wameiegemeza fikra zao potofu?</u>**

**Wanasema kwamba kuthibitisha *ru-yah* inahitajika kwamba Allaah ni *jihah* (muongozo) – na katika mawazo yao, Allaah sio *jihah*. Hivyo wanasema kwamba Allaah sio aidha ndani ya Uumbaji wala nje ya Uumbaji, wala juu wala chini, wala kulia wala kushoto.**

**21) <u>Je, ni athari gani kimantiki zinapatikana kwa yale wanayosema makundi haya mapotofu?</u>**

**Athari za kimantiki zinazopatikana kwa wanayosema ni kwamba Allaah wanamtambua kuwa ni *ma'duum* (asiye kuwepo) – Allaah Ametakasika juu ya haya wanayoyasema!**

**22) <u>Je, Ashaa'irah wanasemaje kuhusiana na *ru-yah*?</u>**

**Dhehebu hili potofu linathibitisha kwamba *ru-yah*, kusema kwamba Allaah ataonekana Siku ya Hesabu, lakini ataonekana bila ya *jihah*. Hii ni fikra ya kijinga, kwani hakuna hata kitu kimoja kinachoonekana ambacho hakipo katika *jihah*. Kwa sababu hii, Mu'tazilah wakazikataa fikra za Ashaa'irah kwani fikra hii ya Ashaa'irah ni kitu kisichoeleweka.**

23) **<u>Je, watu wa *Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah* wanajibu vipi fikra za uongo za makundi matatu haya yaliyotajwa hapo juu?</u>**

**Watu wa *Sunnah* wanasema kwamba Allaah, Mtukufu Asiyekuwa na doa ataonekana Siku ya Hesabu, na Atakuwa katika *jihaad* (muongozo) wa utukufu na ufalme juu ya wote.**

24) **<u>Ni ipi I*ymaan* ya *Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah* kuhusiana na mada ya Allaah kuwa na *jihah*?</u>**

***Jihah* ya Allaah sio ile *jihah* ya Uumbaji. Kinachomaanishwa kwa *jihah* ambayo *jihah* imethibitishwa na Allaah ni ule utukufu wa Allaah juu ya Uumbaji – kwani Allaah ni Mtukufu na yupo juu ya Mbingu zote.**

**Kitabu cha Allaah hakithibitishi wala kukataa 'jihah' ya Allaah, hivyo pale neno hili 'jihah' linapotumika, ni lazima yatumike maelezo yaliyotajwa hapo juu.**

25) **<u>Je, ni uelewa upi sahihi wa Aayah ambayo Shaykh ameinukuu ndani ya Suuratul-An'aam (6:103)?</u>**

Uoni wa watu hautomdiriki (kumhusisha Yeye). **[Suuratul-An'aam (6) aayah 103].**

**Aayah hii inatumika (vibaya) kama ni ushahidi wa baadhi ya watu kukataa *ru-yah* ya Allaah.**

**Hii inamaanisha kwamba: hawatoweza kumhusisha Yeye. Haina maana kwamba: hawatoweza kumuona Yeye, kwa sababu Allaah, Mtukufu na Mfalme, hajasema: uoni wa watu hautaweza kumuona Yeye. Hivyo, *al-idraa* (kuhusisha) kitu na kuona kitu ni vitu viwili tofauti. Hivyo, uoni wa watu utamuona [Aakhirah] Allaah bila ya kumhusisha Yeye.**

26) **<u>Ni maana gani sahihi ya ufahamu wa Aayah ambayo Shaykh ameinukuu ndani ya Suuratul-A'raaf (7:143)?</u>**

Yeye Muusa alisema: "Mola wangu! Nionyeshe (nafsi Yako) ili Nikuone." Akasema (Allaah): "Hutaniona." **[Suuratul-A'raaf (7) Aayah 143]**

**Aayah hii pia inatumika (sivyo) kama ni ushahidi wa baadhi ya watu kukana *ru-yah* ya Allaah.**

**Watu wa *Sunnah* wamejibu kwa kusema: tamko hili la Allaah – Hutaniona – inamaanisha hapa duniani tu. Muusa ('Alayhis Salaam) alikuwa akiuliza kwa Allaah hapa duniani na hakuna yeyote, hata Mitume, watakaoweza kumuona Allaah hapa duniani.**

**Ama kwa Siku ya Hesabu, hakuna shaka yoyote kwamba Waumini watamuona Allaah kweli kweli.**

## Wiki 3 Nukta 22-27



### Maswali Kuhusu Qur-aan

Swali: 1. Tamko zipi kati ya zifuatazo kuhusu Qur-aan ni sahihi?

1. Qur-aan ni kiumbe cha Allaah.
2. Qur-aan haitenganishwi kwa Allaah, na ni kutoka Matamko ya Allaah ambayo ni moja wapo ya Sifa Yake.
3. Jibriyl ameichukua Qur-aan kutoka Lawhul Mahfuudh (sehemu takatifu)
4. Hakuna kosa lolote kwa kusema kwamba usomaji wa mtu katika Qur-aan umeumbwa.

**Jibu: 2. Angalia jibu linalofuata.**

Swali: 2. Ni usemi wa uzushi kutaja kwamba Qur-aan imeumbwa.

Ni Imaam yupi kati ya hawa wafuatao waliadhibiwa na viongozi wa Waislamu kutokana na kukataa kukubali usemi wa uzushi huu?

1. Abu Haniyfah
2. Maalik
3. Ash-Shaafi'iy
4. Ahmad

**Jibu: 4. Adhabu aliyofanyiwa iliitwa *mihnah*.**

Swali: 3. Iwapo mtu atasema kwamba Qur-aan imeumbwa, Je, ni sifa ipi ya Allaah itakuwa wameikataa?

1. Usemi wa Allaah
2. Usikivu wa Allaah
3. Hikmah za Allaah
4. 'Ilmu ya Allaah

**Jibu: 1. Alipoulizwa kuhusu Qur-aan, Imaam Ahmad amesema: "Maneno ya Allaah, yenye kudumu, hayajaumbwa." Angalia 'Misingi Ya Sunnah', ukurasa 92.**

Swali: 4. Ni kundi lipi potofu linaloshikamana na *Iymaan* kwamba Qur-aan imeumbwa?

1. Mu'tazilah
2. Khawaarij
3. Shi'ah
4. Jahmiyyah

**Jibu: 1 na 4.**

Swali: 5. Kuna athari gani za kusema kwamba Qur-aan imeumbwa?

1. Itamaanisha kwamba hakuna maneno ya Allaah yanayoweza kuthibitisha juu ya uumbaji.
2. Inamaanisha kwamba huyo unayemuabudia hawezi kuzungumza na hii ni kasoro inayohusishwa kwa Allaah.
3. Qur-aan inakufa.

**Jibu: zote hizo.**

**Ama kwa 1, Shaykh Swaalih al-Fawzaan amesema: "Hivyo iwapo hakuna maneno ya Allaah yaliyoshushwa kwa Watumwa Wake, kwa hilo basi itawezekana kuthibitisha (hujjah) dhidi yao? ... Iwapo hakuna sehemu yoyote inayoweza kupatikana Maneno ya Allaah – sio ndani ya Tawraat, wala Injiyl, wala Qur-aan – basi hii inamaanisha kwamba ushahidi kutoka**

**kwa Allaah haujasimamishwa juu ya Viumbe – na hili ni kufru kubwa kabisa na upotofu mbaya sana." [Ufafanuzi wa Al-'Aqiydah at-Twahaawiyyah, nukta 50].**

**Ama kwa 2, Shaykh Swaalih al-Fawzaan amesema: "Hatusemi, 'Qur-aan ni kitu kilichoumbwa' ambayo ndiyo wanayosema Jahmiyyah. Hii ni kufru na kukataa Maneno ya Allaah, na kumhusisha Allaah kuwa na kasoro, na kwamba Yeye hazungumzi, na yule asiyezungumza ana kasoro, na haiwezekani yeye kuwa ni *ilaah* (kitu kinachoweza kuabudiwa)." Ufafanuzi wa Al-'Aqiydah at-Tahawiyyah, nukta 130.**

**Ama kwa 3, hii ni hoja kutoka kwa Imaam Ahmad aliyotumia mbele ya mtawala wa Waislamu kumuonesha athari ya kusema kwamba Qur-aan imeumbwa – kwa sababu kila kinachoumbwa kinakufa. Angalia 'Misingi Ya Sunnah', ukurasa 93.**

---

Swali: 6. Mnyororo upi wa ufikishaji Qur-aan ni sahihi?

---

**Jibu: Shaykh Swaalih al-Fawzaan amesema: "Allaah amezungumza nayo, na Jibriyl akaichukua kutoka kwa Allaah, na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) akaichukua kutoka kwa Jibriyl ('Alayhis Salaam), na Ummah ukaichukua kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam)." [Ufafanuzi wa Al-'Aqiydah at-Twahaawiyyah, nukta 45].**

---

Swali: 7. Ni kwa namna gani Jahmiyyah na Mu'tazilah wanatofautiana katika mnyororo wa ufikishaji [Qur-aan]?

1. Hawaamini kwamba Jibriyl alikuwa ni mfikishaji wa Qur-aan kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam).
2. Hawaamini kwamba Allaah alizungumza Qur-aan
3. Wanasema kwamba Jibriyl aliichukua moja kwa moja kutoka *Al-Lawhul Mahfuudh* (sehemu takatifu).

---

**Jibu: 2 na 3.**

**Shaykh Swaalih al-Fawzaan amesema: "Hivyo yeyote anayesema: 'Hakika Jibriyl ameichukua kutoka *Al-Lawhlu Mahfuudh*,' au, 'Allaah ameiumba ndani ya kitu fulani na Jibriyl akaichukua kutoka hicho kitu,' basi mtu huyu hajamuamini Allaah, Mtukufu na Mpole, akiwa na *Iymaan* itakayomtoa nje ya Diyn. Na hii ni kama vile wanavyosema Jahmiyyah na Mu'tazilah na yeyote atakayefuata njia yao." [Ufafanuzi wa Al-'Aqiydah at-Twahaawiyyah, nukta 45].**

Swali: 8. Ni matamko yepi kati ya yafuatayo kuhusu Qur-aan ni maneno ya uzushi, ambazo baadhi yake watu wa uzushi wametumia kuficha uzushi wao?

1. Qur-aan imeumbwa.
2. Maneno ya Qur-aan yameumbwa, lakini maana zake zinatoka kwa Allaah.
3. Qur-aan ni Neno la Allaah, lakini usomaji wetu umeumbwa.
4. Qur-aan ni Neno la Allaah, lakini linahusishwa kwa Allaah ili kuongeza uzuri tu.
5. 'Sijui iwapo Qur-aan ni au si Neno la Allaah.'

**Jibu: Zote hizo. Matamshi haya yanaweza kupatikana ndani ya 'Misingi Ya Sunnah' na Ufafanuzi wa Al-'Aqiydah at-Twahaawiyyah cha Shaykh Swaalih al-Fawzaan**

## Maswali Kuhusu Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) Kumuona Allaah (Subhaanahu wa Ta'ala)

Swali: 9. Ni matamko gani sahihi kuhusiana na hili?

1. Maswahaabah hawakupatapo kutofautiana katika *'Aqiydah* zao.
2. Simulizi tofauti za Maswahaabah zinaweza kukusanywa katika maana yake kisarufi.
3. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) alimuona Allaah ndani ya dunia hii, kwa macho yake, akiwa hajalala.

---

**Jibu: 1 na 2.**

**Ama kwa 1, Shaykh Swaalih al-Fawzaan amesema: "... hakujapatapo kutokezea miongoni mwa (Salaf) tofauti yoyote ya mawazo katika jambo la 'Aqiydah, isipokuwa 'Aqiydah yao ilikuwa moja." [Mwanzo mwa 'Aqiydatut-Tawhiyd].**

**Ama kwa 2, Ibn Hajar amesema kwamba haiwezekani kuunganisha simulizi zinazosema kwamba Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amemuona Allaah kwa moyo wake na sio kwa macho yake. Simulizi zinaweza pia kuunganishwa kwa kusema kwamba yeye (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amemuona Allaah akiwa macho, lakini akiwa hajaamka. Angalia hadidu za chini za 'Misingi Ya Sunnah', ukurasa 21.**

**Ama kwa 3, Imaam al-Barbahariy amesema: "Yeyote anayedai kumuona Mola wake ndani ya dunia hii ni mtu asiyemuamini Allaah, Mtukufu na Mkarimu." Sharhus Sunnah (Ufafanuzi wa *Iymaan*) nukta 51. Darsa zote kamilifu za kusikiliza zinaweza kupatikana katika www.ittibaa.com**

---

## Maswali Ya Ziada Kuhusu Baadhi ya Madhehebu Potofu Yanayoendelea Kutajwa

**(Mengi ya majibu yamechukuliwa kutoka kitabu cha 'Mtazamo Kwa Ufupi Katika Madhehebu Potofu'** ***A Glimpse at the Deviated Sects*** **cha Shaykh Swaalih al-Fawzaan.)**

Swali: 10. Ni madhehebu gani kati ya yafuatayo manne kwa haraka ni misingi ya madhehebu yote?

1. Shi'ah
2. *Qadariyyah*
3. Ikhwaanul-Muslimuun
4. Khawaarij
5. Jahmiyyah
6. Suufiyyah

---

**Jibu:** ***Qadariyyah*****, Khawaarij, Shi'ah, Jahmiyyah.**

**Lakini madhehebu yote haya yamegawanyika zaidi.**

**"Hii ndio hali ya wote wanaoacha Ukweli. Hawaachi kutofautiana na kugawanyika. Yeye, Mtukufu, amesema:** "Basi wakiamini kama mnavyoamini (nyinyi), itakuwa kweli wameongoka. Na wakikengeuka basi wao wamo katika upinzani tu. Basi Allaah atakukinga na shari yao, na Yeye ndiye Askiaye (na) Ajuaye." **[Suuratul-Baqarah: 137]" Shaykh Swaalih al-Fawzaan, Mtazamo Kwa Ufupit Katika Madhehebu Potofu, ukurasa 39.**

---

Swali: 11. Linganisha dhehebu (upande wa kushoto) kwa baadhi ya *Iymaan* zao (upande wa kulia).

| | |
|---|---|
| ***Qadariyyah*** | mapinduzi dhidi ya mtawala |
| | mtenda dhambi mkuu ni kafiri |
| | kuhalalilalisha umwagaji damu ya Waislamu |
| ***Khawaarij*** | kukataa Majina na Sifa za Allaah |
| ***Shi'ah*** | kukataa Q*adar* |
| ***Jahmiyyah*** | kuwachukia Maswahaabah |
| | kumtukuza 'Aliy (Radhiya Allaahu 'anhu) |
| ***Mu'tazilah*** | wanathibitisha Majina |
| | wanakana Sifa za Allaah, isipokuwa kwa saba kati yake |
| ***Ashaa'irah*** | wanathibitisha Majina ya Allaah |
| | wanakataa sifa zote za Allaah |

**Jibu:**

| | |
|---|---|
| ***Qadariyyah*** | **kukataa Q*adar*** |
| | |
| ***Khawaarij*** | **mapinduzi dhidi ya mtawala** |
| | **mtenda dhambi kuu ni kafiri** |
| | **kuhalalisha umwagaji damu ya Waislamu** |
| | |
| ***Shi'ah*** | **kuwachukia Maswahaabah** |
| | **kumtukuza 'Aliy (Radhiya Allaahu 'anhu)** |
| | |
| ***Jahmiyyah*** | **kukataa Majina na Sifa za Allaah** |
| | |
| ***Mu'tazilah*** | **wanathibitisha Majina** |
| | **wanakataa sifa zote za Allaah** |
| | |
| ***Ashaa'irah*** | **wanakana Sifa za Allaah, isipokuwa kwa saba kati yake** |
| | **wanathibitisha Majina ya Allaah** |
| | |

Swali: 12. Linganisha dhehebu potofu kwa muasisi wake.

| | |
|---|---|
| *Khawaarij* | Ibn Kulaab |
| | Wanahusishwa kimakosa na Abul-Hasan al-Asha'ariy, tokea alipotubu *Iymaan* zake potofu, na kuwa miongoni mwa *Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah* |
| *Shi'a* | Jahm ibn Safwaan |
| | ambaye mstari wake wa walimu unarudi nyuma hadi kwa Labiyd, Myahudi aliyemfanyia uchawi Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) |
| *Jahmiyyah* | 'Abdullah ibn Sabaa (Myahudi) |
| | Alianzisha kipindi ambacho 'Uthmaan alikuwa bado ni Khaliyfah |
| *Mu'tazilah* | Dhul Khawaisarah |
| | aliyejadilina na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) |
| | Kipindi cha 'Uthmaan walimfanyia mapinduzi na kumuua. Wameendelea hivyo tokea kipindi hicho. |
| *Ashaa'irah* | Waaswil ibn 'Ataa |
| | aliyeacha mkusanyika wa al-Hasan al-Basriy |
| | baada ya kujadiliana naye kuhusiana na hukumu ya Kiislamu juu ya mtenda dhambi kuu |

**Jibu:**

| | |
|---|---|
| **Khawaarij** | **Dhul Khawaisarah** |
| | **aliyejadilina na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam)** |
| | **Kipindi cha 'Uthmaan walimfanyia mapinduzi na kumuua. Wameendelea hivyo tokea kipindi hicho.** |
| | |
| **Shi'ah** | **'Abdullah ibn Sabaa (Myahudi)** |
| | **Aliuanzisha (Ushia) kipindi ambacho 'Uthmaan alikuwa bado ni Khaliyfah** |
| | |
| **Jahmiyyah** | **Jahm ibn Safwaan** |
| | **Ambaye mstari wake wa walimu unarudi nyuma hadi kwa Labiyd, Myahudi aliyemfanyia uchawi Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam)** |
| | |
| **Mu'tazilah** | **Waasil ibn 'Ataa** |
| | **Aliyeacha mkusanyika wa al-Hasan al-Basriy baada ya kujadiliana naye kuhusiana na hukumu ya Kiislamu juu ya** |

| | |
|---|---|
| | **mtenda dhambi kuu** |
| | |
| **Ashaa'irah** | **Ibn Kulaab** |
| **Page 27** | **Wanahusishwa kimakosa na Abul-Hasan al-Asha'ari, tokea alipotubu *Iymaan* zake potofu, na kuwa miongoni mwa *Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah*** |

## Wiki 5 Nukta 28-36



### Maswali Ya Nukta 28-35 Kuhusu Qiyaamah

S1. Ni zipi kati ya zifuatazo zitapimwa katika *miyzaan* ya Qiyaamah?

1. Matendo
2. Watu
3. Muenekano wa umbile
4. Hati ya kuvingirisha *scrolls*

**Jibu: 1, 2, na 4. Rejeo zifuatazo zimechukuliwa kutoka Ufafanuzi wa *Iymaan* Yenye Kutosheleza cha Shaykh al-'Uthaymiyn, ukurasa 134-136**

**Ama kwa 1, ndani ya Qur-aan inaelezwa:** "Ama wale ambao *miyzaan* ya 'amali zao (nzuri) itakuwa nzito, hao ndio wenye kufaulu; na wale ambao *miyzaan* yao itakuwa nyepesi, hao ndio waliozitia hasarani nafsi zao, na katika Jahnnam watakaa milele." **[Al-Mu'minuun: 102-103].**

**Ama kwa 2, Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) ametueleza:** "Hakika, mtu mnene kabisa ataletwa Qiyaamah na wala hatozidi uzito wa ubawa wa mbu kwa mujibu wa vipimo vya Allaah." **Kisha akasema: "Soma:** "Na wala Hatutavitia uzani Siku ya Qiyaamah." **[Al-Kahf: 105; Al-Bukhaariy na Muslim].**

**Ama kwa 4, ndani ya Hadiyth kuhusu mtu mwenye hati ya kuvingirisha *scrolls*, Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema:** "Kisha kumbukumbu (zenye matendo maovu) zitawekwa katika uzani mmoja na Hati (yenye maneno ya laa ilaaha illa Llaah) yatawekwa katika uzani mwengine..." **[Imepokewa na At-Tirmidhiy na Ibn Maajah]**

S2. Ni kadhia gani ya kuyapima matendo ya asiyeamini?

1. Matendo yake maovu yatayazidi matendo yake mema, hata kama atakuwa na matendo mema ya aina gani.
2. Hana matendo mema.

---

**Jibu: 2. Shaykh Swaalih al-Fawzaan amesema ndani ya Ufafanuzi wa Twahaawiyyah (nukta 172):**

**"Ama kwa asiyeamini, yeye atadhani kwamba matendo mema yanapimwa dhidi ya matendo maovu. Lakini ukweli ni kwamba watashuhudia maovu yao na kutoamini kwao, kwa sababu wao katika hali halisi hawana matendo mema." Angalia** www.ittibaa.com **kwa kusikiliza kipande kamilifu katika lugha ya Kiingereza.**

---

S3. Yepi kati ya matamko ya Allaah yafuatayo ni sahihi kuhusu?

1. Allaah hakupatapo kuzungumza na mtu yeyote hapa duniani.
2. Allaah anazungumza kwa kupitia mfikishaji, yaani Malaaikah.
3. Allaah atazungumza na kila mtu katika Siku ya Hesabu.
4. Baadhi ya watu watahitaji mkalimani baina yao na Allaah.

---

**Jibu: 3.**

**Ama kwa 1 na 2, Allaah amezungumza na Muusa ('Alayhis Salaam) bila ya Malaaikah, kama ilivyoelezwa ndani ya Suuratun-Nisaa Aayah ya 164.**

**Ama kwa 3 na 4, ndani ya Hadiyth iliyosimuliwa na 'Adiy ibn Haatim (Radhiya Allaahu 'anhu):** "Hakuna hata mmoja kati yenu isipokuwa kwamba Allaah Atazungumza naye Siku ya Hesabu, bila ya kuwepo mkalimani baina Yake na yeye. Kisha ataangalia kuliani mwake na kutoona isipokuwa yale aliyoyachuma (matendo yake), kisha ataangalia kushotoni mwake na kutoona isipokuwa yale aliyoyachuma, kisha ataangalia mbeleni mwake na Moto utakuwa unamuangalia yeye, hivyo yeyote miongoni mwenu anayeweza kuokoa uso wake kutokana na Moto, hata kama itakuwa kwa kipande cha tende, basi na afanye hivyo." **[Al-Bukhariy na Muslim]. Angalia hadidu za chini za 'Misingi Ya Sunnah'.**

---

S4. Haya ni matamko kuhusiana na *hawdh* (bwawa). Kwa kila moja, sema iwapo ni kweli au sikweli.

1. Maji yake ni tofauti na maji ya Peponi.
2. Maji yake yanatambuliwa kuwa ni safi, kama maji ya dunia hii.
3. Vyombo vyake ni kama sayari katika anga.
4. Upana wake ni msafara wa mwaka mzima.
5. Mito miwili itapita ndani yake kutoka kawthar, iliyotengenezwa kwa dhahabu.
6. Hakuna Mtume mwengine yeyote atakayekuwa na *hawdh* isipokuwa Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam).
7. Haitahudhurishwa hadi baada ya kuhesabiwa.

---

**Jibu: Zote sikweli. Hapa chini ni baadhi ya simulizi kuhusiana na *hawdh*.**

**Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema:** "Ninaapa, kwa Allaah, kwamba mimi ninaangalia *hawdh* yangu sasa hivi." **[Al-Bukhaariy]**

**Yeye (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema:** "Yeye (Allaah) atanipatia *al-kawthar*, na mto wake ni kama Pepo unaoelea ndani ya *hawdh*." **[Ahmad]**

**Yeye (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema:** "Hakika, kwa kila Mtume kutakuwa na *hawdh*. Na hakika watashindana kwa mnasaba wa nani ambao utaufikia watu wengi. Na ninatarajia mimi nitakuwa na (mto) ambao wenye kufikiwa na (watu) wengi." **[At-Tirmidhiy]**

**Yeye (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema:** "*Hawdh* yangu ni mpana kama vile msafara wa mwezi mmoja; maji yake ni meupe kuliko maziwa, harufu yake ni burudisho kuliko miski na vyombo vyake vya kunywea ni kama vile nyota za mbingu; yeyote anayekunywa kutokana na mto huu hatahisi kiu daima." **[Al-Bukhaariy na Muslim]**

**Ukweli wa kwamba kuna mito miwili inayoingia kutoka *kawthar* (mto uliopo Peponi), mmoja wa fedha na mwengine wa dhahabu, umechukuliwa kutoka *Hadiyth* mbili za Swahih ya Muslim.**

**Ukweli wa kwamba maji yake ni matamu kuliko asali - umechukuliwa kutoka *Hadiyth* iliyomo ndani ya Sunan ya At-Tirmidhiy iliyotajwa kuwa**

**ni sahihi na Shaykh al-Albaaniy.**

S5. Ni nani atakayeekwa mbali na *hawdh*, kama ilivyotajwa ndani ya *Hadiyth* sahihi iliyosimuliwa na al-Bukhaariy ndani ya Swahiyh yake?

1. Wasioamini
2. Wazushi
3. Waovu

**Jibu: 2.**

**Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) atamuuliza Allaah kuhusiana na hili, akisema:**

"Ee Mola wangu, (wao wanatoka katika) Ummah wangu, Ummah wangu!"

Allaah, Mtukufu na Mkarimu atajibu:

"Hakika hujui ni kipi walichoanzisha/walichozua baada yako!"

Hivyo (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) atasema:

"Kuwa mbali, mbali kabisa na yule ambaye amebadilisha na kugeuza!"

**[Hadiyth imesimuliwa na al-Bukhaariy (namba 6582) na Muslim].**

S6. Matamko gani kati ya yafuatayo ni kweli?

1. *Hadiyth* kuhusu *hawdh* ni *mutawaatir*.
2. Kuna maafikiano ya *Salaf* kuhusu kuwepo *hawdh.*
3. Hata Mu'tazilah wanathibisha (kuwepo) *hawdh*.

**Jibu: 1 na 2. Angalia hadidu za chini kutoka 'Misingi Ya Sunnah'.**

S7. Ni nani anaweza kuadhibiwa ndani ya kaburi?

1. Ni wale wasioamini tu.

2. Wasioamini na Waislamu waovu.
3. Watu waliotenda madhambi makubwa kabisa.
4. Ni roho tu zitakazoadhibiwa na sio miili.

---

**Jibu: 2.**

**Ama kwa wasioamini, basi Yeye, Mtukufu na Mkarimu, anasema kuhusu watu wa Fir'awn:**

"Adhabu za Motoni wanadhihirishiwa (makaburini mwao) asubuhi na jioni. Na siku ile kitakapotokea Qiyaamah (kutasemwa): "Waingizeni watu wa Fir'awn katika adhabu kali zaidi (kuliko hii waliyoipata kaburini)." **[Al-Mu'minuun: 46]**

**Ama kwa Waislamu waliotenda madhambi madogo kuliko madhambi makubwa, basi Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) alipita baina ya makaburi mawili na kusema:**

"Hakika hawa wawili wanaadhibiwa na wala hawaadhibiwi kwa jambo kubwa. Isipokuwa ni jambo kubwa – au, hakika ni jambo kubwa. Ama kwa mmoja wao, alikuwa akifanya *namiimah* (visa vya kusababisha ugomvi baina ya watu). Ama kwa mwengine, alikuwa hajihifadhi kutokana na mkojo wake." **[*Hadiyth* imesimuliwa na Al-Bukhaariy na Muslim kutoka Hadiyth na ibn Abbaas (Radhiya Allaahu 'anhuma)].**

**Ama kwa 4, basi Shaykh al-'Uthaymiyn amesema ndani ya Ufafanuzi wa *Iymaan* Yenye Kutosheleza, ukurasa 127: Shaykh ul-Islaam Ibn Taymiyyah amesema: "Fikra ya *Salaf* na wanachuoni wa Ummah huu ni kwamba adhabu au starehe zinatokea juu ya roho na mwili wa maiti."**

---

S8. Matamko yafuatayo ni kuhusiana na watu wanaokana adhabu ya kaburi. Ni zipi kweli au sikweli?

1. Wanakataa simulizi za mutawaatir kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam).
2. Wanasema kwamba baadhi ya matamko kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) yanaweza kukubalina na mengine hayawezi kuchukuliwa kama ni mambo ya *Iymaan*.
3. Wanakataa makubaliano ya *Salaf*.

---

**Jibu: 1, 2, na 3. Angalia Ufafanuzi wa *Iymaan* Yenye Kutosheleza cha**

**Shaykh al-'Uthaymiyn na Ufafanuzi wa Twahaawiyyah cha Shayh al-Fawzaan.**

S9. Wanafiki watajibu vipi kwa Maswali matatu yatakayoulizwa ndani ya kaburi?

1. Ataweza kuyajibu, kama alivyokuwa akiweza kuyajibu hapa duniani.
2. Hatoweza kuyajibu kisahihi, ingawa ataweza kuyajibu kisahihi hapa duniani.
3. Ataweza kuyajibu kisahihi ni nani alikuwa Mola wake, lakini sio Maswali mengine.

**Jibu: 2. Angalia *Hadiyth* ya al-Baraa ibn 'Aazib iliyomo katika Maswali ya mwisho ya wiki hii.**

S10. Matamko gani ni sahihi kuhusu Malaaikah watakaomuuliza mtu ndani ya kaburi?

1. Ni wakali mno.
2. Ni pale tu wanapotokezea ndio roho ya mtu inaruka mbinguni na kurejea.
3. Wao ndio Malaaikah wa mwanzo kuweza kuzungumza na maiti.

**Jibu: 1. Angalia *Hadiyth* ya Baraa ibn 'Aazib (chini).**

S11. Ni nini maana ya S*hafaa'ah* (uombezi) ndani ya *Shari'ah*?

1. Kusuluhisha baina ya makundi mawili yenye kupigana wenyewe kwa wenyewe, kwa ajili ya kuleta amani baina ya makundi hayo mawili.
2. Kusuluhisha baina ya mtu aliye na haja (upande mmoja) na mtu ambaye anayeweza kuitimiza hiyo haja (kwa upande wa pili).
3. Kuwataka Mitume waombe kutoa mazuri na kusamehe maovu, na kuondosha mashaka tunayokutana nayo duniani hapa.

**Jibu 2: Shaykh al-Fawzaan amesema, ndani ya Ufafanuzi wa**

**Twahaawiyyah (nukta 84): "Ina maana ya kujibu haja, na kusuluhisha baina ya mtu aliyekuwa na haja kwa yule ambaye anayeweza kuitimiza hiyo haja."**

S12. Zipi zifuatazo ni sharti mbili zilitojwa mahsusi kwa wanachuoni, kwa (kuomba) kukubaliwa uombezi mbele ya Allaah?

1. Yule anayeomba msamaha hali ya kuwa ni mtu mzima.
2. Allaah anatoa ruhusa kwa uombezi kutokea.
3. Yule anayeombewa msamaha ni mtu ambaye Allaah ameridhika naye.
4. Yule anayeombewa msamaha si mtu mwenye madhambi makubwa.

**Jibu: 2 na 3. Muhammad ibn Abdil-Wahhaab amesema ndani ya 'Misingi Mikuu Minne': "Na uhakika wa usamehevu ni kwa kile kinachoombewa kutoka kwa Allaah, ilhali yule anayeomba ametunukiwa kuombea msamaha, na yule anayeombewa ni mtu ambaye matendo na maneno yake yanamridhia Allaah, baada ya kutoa ruhusa, kama Yeye, Mtukufu, alivyosema:** "Na nani huyo awezaye kuombea mbele Yake (Mungu) bila ya idhini Yake?" **[Al-Baqarah: 255]**

S13. Kuhusiana na uombezi, zipi kati ya zifuatazo ni sahihi?

1. Mitume, Malaaikah na watu waongofu ndio pekee watakaoweza kuomba msamaha.
2. Asiyeamini hataruhusiwa kuombewa msamaha.
3. Hakutakuwa na usamehevu hadi pale hukumu zitakapokamilika.
4. Watu wa Jannah hawataingia Jannah hadi waombewe msamaha.

**Jibu: 4. Angalia Ufafanuzi wa Twahaawiyyah cha Shaykh al-Fawzaan. Hapa chini ni baadhi ya nukta zilizochukuliwa kutoka Nukta 84.**

**Ama kwa 1, basi *afraat* (watoto waliofariki kabla ya kufikia umri wa baleghe) pia wataweza kuwaombea msamaha wazee wao.**

**Ama kwa 2, Abu Twaalib ndiye atakayekuwa pekee kati ya wasioamini kuweza kukubaliwa kuombewa msamaha, lakini hatatolewa nje ya Moto. Usamehevu wake utakuwa wa kufanyiwa tahfifu katika adhabu yake.**

**Ama kwa 3, basi hukumu ya baina ya watu wawili haitokamilika hadi**

**Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) atakapowaombea msamaha watu. Huu ndio uombezi mkubwa.**

**Ama kwa 4, Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) atawaombea msamaha watu wa Peponi kwa uhakika kuingia Peponi. (Ama kwa wasimulizi mmoja mmoja, basi hawakuelezwa wote na Shaykh ndani ya kitabu hichi).**

## Maswali Ya Nukta 35-36 Kuhusu Dajjaal

**Maswali yote yamechukuliwa kutoka simulizi zilizosahihishwa na Shaykh Al-Albaaniy ndani ya kitabu chake kuhusu mada hii.**

S14. Zipi kati ya maelezo yafuatayo ni sahihi kuhusu Dajjaal (Masiyh wa uongo)?

1. Hivi sasa yupo hai, na alikuwa yuhai tokea wakati wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam).
2. Atakuwa juu ya ardhi kwa miaka isiyozidi miwili.
3. Atayayuka kwa muonekano wa 'Iysa ('Alayhis Salaam), na hichi ndicho kitu kitakachomuua.

**Jibu: 1 na 2.**

S15. Dajjaal atainuka (atatokezea kwa mara ya kwanza) wapi?

1. Pande za Magharibi.
2. Pande za Mashariki.
3. Eneo lisilotambulikana.
4. Jerusalem.

**Jibu: 2. Atatokezea kutoka katika maeneo ya baina ya ash-Shaam na Iraaq.**

S16. Zipi kati ya zifuatazo ni sifa zake zinazomtenganisha na wengine?

1. Ana nywele za rangi ya udongo zilizonyooka.
2. Ana jicho moja.
3. Ana neno 'mushrik' lilioandikwa baina ya macho yake.
4. Ataiamuru mvua kwa uwezo wa Allaah.
5. Atakuwa na uwezo wa kuwafufua wafu na kuweleta duniani.
6. Atakuwa mrefu.

**Jibu: 2, 4 na 5.**

**Atakuwa na nywele rangi ya udongo zilizosokotana. Atakuwa na neno 'kaafir' lililoandikwa baina ya macho yake. Atakuwa mfupi.**

S17. Yepi yafuatayo ni kweli kuhusu wafuasi wa Dajjaal?

1. Kutakuwa na Mayahudi wengi miongoni mwao.
2. Kutakuwa na wanawake wengi miongoni mwao.

**Jibu: zote hizo.**

**Hadiyth ya al-Baraa ibn Aazib iliyosimuliwa na Ahmad, Abu Daawud, al-Haakim na wengineo.**

**Yafuatayo ni maneno ya Imaam Ahmad (Rahimahu Allaah) ikiwa imeengezewa maelezo sahihi kutoka kwa wengine, yaliyokusanywa na kusahihishwa na Shaykh Al-Albaaniy (Rahimahu Allaah) ndani ya 'Ahkaamul-Janaa'iz (ukurasa 198-202) na ipo katika kiwango cha Imaam al-Bukhaariy na Muslim**

'Tulienda nje pamoja na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) katika mazishi ya mtu mmoja wa Answaar. Hivyo tukapita katika Jeneza na yeye (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) alikuwa na kijiti, ambacho alikuwa akichipulia ardhi (mfano wa fimbo ya mkononi). Akaanza kuangalia mbinguni, na kuangalia ardhini, na kuinua muono wake na kuinamisha mara tatu, na kisha kusema:

Ombeni hifadhi kutoka kwa Allaah kutokana na Adhabu ya Kaburi!

… mara mbili au mara tatu,

na kisha yeye (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) akasema:

Ewe Allaah, ninaomba hifadhi yako kutokana na Adhabu za Kaburi.

… mara tatu,

Na kisha yeye (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) akasema:

Mja muumini, anapoondoka duniani hapa na kuelekea Aakhirah – basi baadhi ya Malaaikah kutoka mbinguni wanamsitiri, kwa uso mweupe na zile nyuso zao zikiwa [zinangara kama] ni jua. Pamoja nao, kuna guo la kujifunikia kutoka katika maguo ya Peponi na mafuta mazuri ya kujifukiza kutoka mafuta mazuri ya Peponi – kutoka pale anapoweza kuonekana hadi walipokaa naye.

Na kisha Malaaikatul-Mawt ('Alayhis Salaam) anakuja, kisha anakaa baina ya kichwa chake na kusema:

Ewe roho safi! (na katika mapokezi mengine – iliyopumzika), njoo katika msamaha wa Allaah na Ridhaa Yake! Hivyo inatoka na kuruka kama vile tone la maji linapodondoka nje ya chombo.

Hivyo yeye ('Alayhis Salaam) ataichukua – na katika pokezi moja – pale roho yake itakapotoka, basi kila Malaaikah baina ya Mbingu na Ardhi huiombea dua'a na kila Malaaikah wa Mbinguni na Milango na (chini) ya Peponi hufunguliwa kwa ajili yake.

Na hakuna wakaazi (yaani Malaaikah) atakayekuwepo mlangoni isipokuwa ni kwamba ataiombea dua'a kwa Allaah kwamba roho yake ichukuliwe kutoka muelekeo wao. Hivyo pale (Malaaikatul-Mawt) atakapoichukua, haiachii mkononi hata kwa upweso wa jicho hadi kuichukua na kuiweka katika guo hilo na katika manukato – na hivyo ndivyo Anavyosema, Mtukufu na Mkubwa:

**'Wajumbe wetu wanaichukua roho yake katika Kifo, na wala hawakosei katika wajibu wao.'**

Na harufu kutoka kwake hujitokeza kama vile harufu ya miski safi inavyopatikana katika mgongo wa ardhi. Kisha wanaipeleka juu (roho aminifu) na hawaipeleki kwa yeyote (kundi lolote la Malaaikah) isipokuwa kwamba watasema: Hii ni roho gani safi? Kisha husema: Ni roho fulani na fulani, mtoto wa fulani na fulani.

… wakimtaja kwa majina yake mazuri ambayo alikuwa akiitwa duniani hapa, hadi kumfikisha katika mbingu ya chini kabisa na kuomba ifunguliwe kwa ajili yake – hivyo hufunguliwa kwa ajili yake.

Na kisha baadaye aliye karibu naye kutoka katika kila mbingu hufuatana naye hadi mbingu inayofuata hadi anafika mbingu ya saba – na Allaah, Mtukufu na Mwenye Hikmah husema:

**Andika kumbukumbu za mja Wangu ndani ya *'Illiyyiyn* (mbingu ya juu kabisa)!**

**'Na kitu gani kitakachokujuulisha ni nini *'Illiyyuun*? (ndani yake) kuna kumbukumbu zilizoandikwa. Zinazoshuhudiwa na wale walio karibu walioyaandika.'**

Hivyo yeye (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) atasema:

Kisha kumbukumbu zake zitaandikwa ndani ya *'Illiyyiyn*. Kisha itasemwa:

Mrudishe ardhini, kwani nimewaahidi kwamba: Kutokana nayo nimekuumbeni, na kutokana nayo nitawarejesha, kisha nitawachukua kutokana nayo mara nyengine tena.

Kisha atarudishwa ardhini na roho yake itarejeshwa katika mwili wake, na atasikia milio ya miguu kutoka kwa swahiba zake pale wanapomuacha wakienda zao (kutoka kaburini kwake). Kisha Malaaikah wawili watakuja kwake, na watakuwa ni wakali mno kwake, watamkalisha kitako na watamwambia:

Ni nani Mola wako?

Hivyo atasema: Mola wangu ni Allaah.

Watamwambia: Ni ipi Diyn yako?

Hivyo atasema: Diyn yangu ni Uislaam.

Kisha watamwambia: Alikuwa ni mtu gani huyu aliyeletwa miongoni mwenu?

Atasema: Yeye ni Mjumbe wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam).

Wewe ulijuaje?

Hivyo atasema: Nilisoma Kitabu cha Allaah, na kukiamini, na kukithibitisha.

Kisha atakuwa mkali kwake, na kusema: Ni nani Mola wako? Ni ipi Diyn yako? Ni nani Mtume wako?

Na hii itakuwa ni mtihani wa mwisho atakaokumbana nao.

Hivyo ndivyo alivyosema Allaah, Mtukufu na Mkarimu:

**'Allaah atawafanya waumini kuwa na *qawl thaabit*, miongoni mwa *qawl thaabit* katika maisha ya hapa duniani.'**

Hivyo atasema: Mola wangu ni Allaah, Diyn yangu ni Uislaam na Mtume wangu ni Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam).

Kisha muitaji kutoka mbinguni atanadi:

**‘Mja wangu amezungumza Ukweli, hivyo mpatie kitanda kutoka Peponi, na mpatie kivazi kutoka peponi na mfungulie mlango unaoelekea Peponi.’**

Hivyo pepo zake laini na manukato yake yatakuja kwake, na kaburi lake litapanuliwa kwa ajili yake kwa umbali wa macho yake yatakavyoweza kuona. Na kisha kutakuja (katika simulizi moja, kutaoneshwa kwake) mtu aliyekuwa na sura nzuri maridadi (handsome), akiwa na kivazi kizuri, na lafdhi nzuri, na atasema:

Pokea habari njema ya ile inayokupendeza? Pokea habari njema ya ridhaa kutoka kwa Allaah na bustani zisizokwisha uzuri wake! Hii ni siku yako uliyoahidiwa.

Kisha atamjibu: Na wewe – Allaah akupe bishara njema – wewe ni nani? Sura yako ni sura ambayo inayokuja na mazuri.

Hivyo atasema:

Mimi ni matendo yako mema. Naapa kwa Allaah, sikujui isipokuwa ni kwamba wewe ni mwenye pupa katika kumtii Allaah, mpole katika kumuasi, basi Allaah akulipe mema.

Na kisha mlango utafunguliwa kutoka Peponi na pia mlango kutoka Motoni, na kisha atasema:

Hii ilikuwa iwe ndio sehemu yako, yareti ungelikuwa ni muasi kwa Allaah lakini Allaah Amekupatia mbadala wa hili badala yake.

Na atakapoona kile kilichomo Peponi, atasema: Ewe Mola wangu, iharakishe Saa ili niweze kurudi kwa ukoo wangu nakile kilichotayarishwa kwa ajili yangu!

Hivyo itasemwa kwake: Kuwa na ustahamilivu.

Na yeye (Swalla Allaahu ‘alayhi wa aalihi wa sallam) amesema:

Na kwa kaafir (mtumwa asiyeamini) (na katika simulizi moja – faajir, muovu), pale atakapoachana na dunia hii na kuelekea Aakhirah, basi Malaaikah wanamrithi kutoka Mbinguni – Malaaikah wale walio na ugumu na wakakamavu wenye sura nyeusi, wakiwa na matambara mabaya kabisa kutoka Motoni.

Hivyo watakaa katika sehemu ambayo uoni utamfikia, na kisha Malaaikatul-Mawt atakuja na kukaa kichwani mwake na kusema:

Ewe mpumbavu na roho ovu! Toka uingie katika Maapizo ya Allaah na Ghadhabu Zake!

Hivyo hiyo roho itajikokota kutoka mwilini mwake. Hivyo ataitoa, kama vile ilivyo kwa uma iliyochomwa na ncha nyingi inavyotolewa kutoka kitambaa kilichorowana. Mishipa na misuli itachanwa chanwa pamoja nayo. Na atalaaniwa na kila Malaaikah baina ya Mbingu na Ardhi na kila Malaaikah ndani ya Mbingu.

Milango ya Peponi itafungwa. Hakutakuwa na kiumbe chochote cha mlango wowote isipokuwa ni kwamba anaiombea kwa Allaah kwamba roho yake isipelekwe kupitia upande wao.

Hivyo ataichukua (roho hiyo) na pale atakapoichukua, hataiachia mkononi mwake hata kwa upweso wa jicho – hadi atakapoiweka kwenye tambara bovu. Na kutatoka ndani ya mwili wake harufu kama vile harufu mbaya kabisa ya uozo na mzoga mbovu uliooza ardhini.

Hivyo wataichukua, na hawatapita katika kundi lolote la Malaaikah isipokuwa ni kwamba watasema:

Ni roho gani hii ovu?

Hivyo watasema: Fulani fulani, mtoto wa fulani na fulani.

… wakitaja majina mabaya kabisa ambayo alikuwa akiitwa nayo hapa duniani, hadi kufikia mbingu ya chini kabisa, na ombi linafanywa kwa ajili yake ili ipate kufunguliwa lakini haitafunguliwa kwa ajili yake. Kisha (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) alisoma:

**'Milango ya Mbingu haitafunguliwa kwa ajili yao (wasioamini) wala hawataingia Peponi hadi pale ngamia atakapopita katika tundu ya sindano.'**

Hivyo (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) alisema:

Hivyo Allaah, Mtukufu na Mkarimu atasema:
**Andika kumbukumbu zake katika *Sijjiyn* (ardhi ya chini kabisa)!**

Kisha itasemwa:

**Mrudishe Mtumwa Wangu Ardhini kwa sababu nimewaahidi kwamba kutokana nayo nimewaumba, na kutokana nayo nitawarudisha na kutokana nayo nitawarejesha kwa mara nyingine tena.**

Hivyo roho yake itarushwa kutoka Mbinguni hadi itakapofika ardhini ndani ya mwili wake.

Kisha (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) akasoma:

**'Na yeyote anayemshirikisha Allaah, basi ni kama vile alivyoanguka kutoka Mbinguni na kukamatwa na ndege – au upepo uliomchukua na kumtupa katika sehemu ya mbali kabisa.'**

Hivyo roho yake itarudishwa katika mwili wake na atasikia nyayo za swahiba zake pale watakapoachana naye, na Malaaikah wawili watamjia ambao ni wakali kabisa. Na kutakuwa na ugumu kwake, na watamfanya akae na kumwambia:

Ni nani Mola wako?

Hivyo atasema: Aaah, aaah… sifahamu.

Hivyo watamwambia: Ni ipi dini yako?

Hivyo atasema: Aaah, aah… sifahamu.

Hivyo watamwambia: Hivyo unasemaje kuhusu mtu huyu aliyeletwa miongoni mwenu?

Hatakuwa na uwezo wa kulitaja jina lake.

Hivyo itasemwa: Muhammad.

Hivyo atasema: Aaah, aah… sifahamu. Niliwasikia watu wakisema hivyo.

Itasema: Hufahamu na hukusoma.

Hivyo mnadi kutoka Mbinguni ataita: Amesema uongo. Hivyo mpe makaazi yake kutoka Motoni, na mfungulie mlango wa Motoni.

Hivyo mvuke wake na upepo wake unaochoma utamjia, na kaburi lake litambana hadi mifupa kuelekea upande wa pili. Kisha kutatokea mtu aliyekuwa na uso mbaya kabisa na mwenye nguo mbovu, akiwa na harufu iliyooza na kusema:

Pokea habari ambazo zitakuudhi. Hii ni siku yako uliyoahidiwa.

Hivyo atasema: Na Allaah akupatie wewe habari ovu! Wewe ni nani? Kwani sura yako ni ile ambayo inakuja pamoja na uovu.
Hivyo atasema: Mimi ni matendo yako maovu. Sijakufahamu isipokuwa kwamba wewe ni mpole katika kumtii Allaah, mwenye haraka ya kumuasi, hivyo Allaah akulipe maovu.

Na kisha kutaachiwa wazi kwake (Malaaikah) aliyekuwa kipofu, bubu na kiziwi na atakuwa na nyundo nzito mkononi mwake. Iwapo mlima utapigwa nayo, utakuwa ni vumbi. Hivyo atampiga nayo, hadi kuvurugwa kuwa ni vumbi. Na kisha Allaah atamrudisha kama alivyokuwa kabla, na (kisha) atampiga kwayo tena, na kupiga ukelele ambao utasikiwa na viumbe vyote, isipokuwa binaadamu na majini.

Na kisha mlango utafunguliwa kwa ajili yake kutoka Motoni na makaazi yake yatatoka Motoni.

Hivyo atasema: Ewe Mola wangu, usiifikishe Saa!



## Maswali Kuhusu *Iymaan*

S1. Ni ipi tafsiri ya *Iymaan*?

**Jibu:**

**Ni kukiri kwa ulimi, kuamini kwa moyo, na matendo ya miguu, inaongeza utiifu kwa Allaah, na inapunguza uasi.**

**Rejeo: Khutbah Zenye Manufaa katika Kuthibitisha Ushahidi wa Tawhiyd cha Shaykh Abdil-Wahhaab al-Waswaabiy.**

S2. Ni zipi nguzo sita (arkaan) za *Iymaan*?

**Jibu: "Ni kumuamini Allaah, Malaaikah wake, Vitabu Vyake, Mitume Wake, Siku ya Mwisho, na kwamba unaamini Qadar - mazuri na mabaya yake," kama ilivyo ndani ya Hadiyth ya Jibriyl ('Alayhis Salaam) na Suurah aal 'Imraan (3) Aayah 173.**

S3. Aayah zifuatazo zinatumiwa mahsusi kama ni ushahidi muhimu kwa misingi ya *Iymaan*?

1. Kwamba *Iymaan* ni kutenda kwa moyo.
2. Kwamba *Iymaan* inajumuisha kukiri na kutenda.
3. Kwamba *Iymaan* inaongezeka.
4. Wale (yaani waumini) ambao watu (wanafiki) wanasema: "Walioambiwa na watu: Kuna watu wamekukusanyikieni, waogopeni! Hayo yakawazidishia *Iymaan*, wakasema: Allaah anatutosha, naye ni mbora wa kutegemewa." [Al-'Imraan: 173]
5. "Hakika Waumini ni wale ambao anapotajwa Allaah nyoyo zao hujaa khofu, na wanaposomewa Aayah zake huwazidisha *Iymaan*, na

wakamtegemea Mola wao Mlezi." [Al-Anfaal: 2]
6. "… na wazidi *Iymaan* wale walio amini," [Al-Muddaththir: 31]

---

**Jibu: 3. Rejeo: Khutbah Zenye Manufaa katika kitabu cha Kuthibitisha Ushahidi wa Tawhiyd cha Shaykh al-Waswaabiy.**

**Halikadhalika, Shaykh al-Fawzaan anaeleza ndani ya Ufafanuzi wa Twahaawiyyah nukta 137 kwamba Hadiyth zifuatazo mbili ni ushahidi wa kwamba *Iymaan* inapungua:**

"Yeyote miongoni mwenu anayeona jambo ovu basi na alirekebishe kwa mkono wake, na ikiwa haweze basi kwa ulimi wake, na ikiwa hawezi basi kwa moyo wake na hii ndio *Iymaan* ya chini kabisa." **[Hadiyth ya Abu Sa'iyd al-Khudhriy (Radhiya Allaahu 'anhu) iliyopokewa na Muslim – namba 49]**

**Na katika simulizi:**

"Na hakuna kinachovuka [kwa kulipwa] hata kwa upale wa mbegu [udogo] wa *Iymaan*." **[Hadiyth ya 'Abdullaah ibn Mas'uwd (Radhiya Allaahu 'anhu) iliyopokewa na Muslim – namba 50]**

---

S4. Je, Murji-ah wanaamini vipi kuhusu *Iymaan*?

1. *Iymaan* ni tamko la ulimi, *Iymaan* ya moyo na matendo ya miguu.
2. Matendo sio sehemu ya *Iymaan*.
3. *Iymaan* na *ihsaan* ni kitu kimoja.

---

**Jibu: 2**

**Kuna aina nne za Murji-ah, kama ilivyoelezwa na Shaykh al-Fawzaan ndani ya Ufafanuzi wa Twahaawiyyah nukta 137.**

**a) <u>Hanafiy</u>**
***Iymaan* ni kukiri kwa ulimi na I*ymaan* ndani ya moyo.**

**b) <u>Karraamiyyah</u>**
***Iymaan* ni kukiri kwa ulimi tu.**

**c) <u>Ashaa'irah</u>**
***Iymaan* ni I*ymaan* ndani ya moyo tu.**

**Kwa mujibu wa tafsiri zao, Abu Lahab, Abu Twaalib, na Mayahudi basi wote watatambuliwa kuwa ni waumini kwa sababu wametambua ndani ya mioyo yao kwamba Muhammad (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) alikuwa hakika ni Mjumbe wa Allaah – lakini uadui na kibri viliwazuia kumfuata.**

**d) Jahmiyyah**
***Iymaan* ni kuhamasika (yaani kumuelewa Allaah) ndani ya moyo.**

**Kwa mujibu wa tafsiri zao, Firawn na Ibliys wote wanatambulika kuwa ni waumini kwa sababu walielewa kwamba Allaah Yupo.**

## Maswali Kuhusu Kuacha *Swalah*

S5. Zipi zifuatazo ni sahihi kuhusiana na kuacha *Swalah* kwa uvivu?

1. Wanachuoni wanakubaliana kwamba ni kufr.
2. Wanachuoni wanakubaliana kwamba sio kufr.
3. Wanachuoni wanatofautiana iwapo ni kufr au laa, wakiegemeza maandiko.

**Jibu: 3. Angalia hadidu za chini za 'Misingi Ya Sunnah'.**

**Wanachuoni wanakubaliana kwamba kuacha *Swalah* ni kufr, na kwamba yeyote anayekana ulazima wake ni kaafir – kwa mujibu wa *Ahaadiyth* zilizo wazi. Hata hivyo hawakubaliani kuhusu mtu anayeacha kwa uvivu na mfano wake – Je, anakuwa ni kaafir au laa?**

S6. Je, ni nani aliyesema maneno yafuatayo?

"Maswahaabah wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) hawakupatapo kuelewa chochote miongoni mwa matendo, ambapo kuacha kwake ni kutoamini, zaidi ya *Swalah*."

1. 'Abdullaah bin Shaqiyq, tabi'iy
2. Ibn Taymiyah, Imaam maarufu
3. Usaamah bin Ladin, khaarijiy

**Jibu: 'Abdullaah bin Shaqiyq al-'Uqayliy, Taabi'iy anayeheshimika (Rahimahu Allaah).**

## Maswali Kuhusu Maswahaabah

S7. Ni nani aliyesema maneno yafuatayo?

"Tulikuwa tukisema tukiwa pamoja na Mjumbe wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam): Mtu bora baada ya Mjumbe wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) ni Abu Bakr kisha 'Umar kisha 'Uthmaan. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) alikuwa akisikia hayo na wala hakatai kwa hilo."

1. Ibn 'Umar
2. 'Aliy
3. 'Aaishah

**Jibu: 1. Imepokewa na Al-Bukhaariy ndani ya Swahiyh yake namba 3697 na wengineo.**

S8. *Swahaabah* ambaye anafuata kwa ubora ni 'Aliy bin Abi Twaalib. Je, ni lipi linaweza kusemwa juu ya maneno haya?

1. Ni upotofu kufikiria kitu zaidi ya haya.
2. Baadhi ya *Ahlus-Sunnah* wamesema kwamba 'Aliy ni bora (ana heshimika) kuliko 'Uthmaan. Hawatambuliwi kuwa wamepotoka iwapo watashikilia fikra hii.
3. Hakuna hata mmoja miongoni mwa *Ahlus-Sunnah* waliopingana na fikra kwamba 'Uthmaan alikuwa sahihi kuwa Khaliyfah kabla ya 'Aliy.
4. Mashi'ah wamekwenda njia mbaya katika suala tu ambalo Maswahaabah walikuwa ni wajuzi kuliko wengine, na katika suala ambalo ni nani miongoni mwao awe ni Khaliyfah.

**Jibu: 2 na 3.**

**Ama kwa 1 na 2, Shaykh al-'Uthaymiyn anasema ndani ya maandishi yake ya al-'Aqiydah al-Waasitwiyyah ukurasa 188: "Swahaabah aliye bora kama mmoja ni Abu Bakr, kisha 'Umar kwa mujibu wa makubaliano. Baada yao**

**ni 'Uthmaan kisha 'Aliy, kwa mujibu wa makubaliano ya wengi katika *Ahlus-Sunnah* ambao wameogelea katika suala hili. Baada ya hili, tofauti zikajitokeza katika kutofautisha baina ya 'Aliy na 'Uthmaan. Baadhi walimpendelea 'Uthmaan na wakabaki kimya, wengine wakampendelea 'Aliy kisha 'Uthmaan, na baadhi wakasita kutofautisha. Yule ambaye anashikilia msimamo kwamba 'Aliy ni bora kuliko 'Uthmaan haendi kwenye njia ya upotofu kwa sababu *Ahlus-Sunnah* wamekubaliana na fikra hii."**

**Angalizo kwamba mtu hatotambuliwa kuwa ni mpotofu kwa kushikilia kwamba 'Aliy alikuwa ni bora kuliko 'Uthmaan; hata hivyo atatambuliwa kuwa ni mpotofu iwapo atashikilia kwamba yeye ndiye alitakiwa kuwa ni Khaliyfah badala yake – kwani hili ni kinyume na *ijmaa´* (makubaliano) ya Maswahaabah.**

**Shaykh al-Fawzaan akionesha nukta hii ndani ya Ufafanuzi wa al-Waasitwiyyah (ukurasa 147):**

**"Kwa kufupisha, suala la kutoa hukumu kwa 'Aliy (Radhiya Allaahu 'anhu) juu ya wengine kutoka kwa Makhaliyfah watatu ni kwamba:**

**1) Yeyote anayemtolea hukumu kwa mujibu wa *Khilaafah*, basi amepotoka – kwa makubaliano;**

**2) Yeyote anayemtolea hukumu juu ya Abu Bakr na 'Umar, basi yeye pia amepotoka;**

**3) Na yeyote anayemtolea hukumu juu ya 'Uthmaan kwa kuheshimika, basi yeye hatambuliwi kuwa ni mpotofu, hata iwapo hii ni kinyume na kauli sahihi."**

**Ama kwa 3, katika kurasa inayofuata kwenye kitabu hicho hicho, Shaykh al-'Uthaymiyn amesema: "Yule ambaye anayetofautiana katika Ukhaliyfah wa yeyote miongoni mwao au katika mtiririko wake amekwenda katika upotovu kwa sababu ni kinyume na makubaliano ya Maswahaabah na makubaliano ya *Ahlus-Sunnah*."**

**Rudia pia Al-´Aqiydat al-Waasitwiyyah cha Shaykh Islaam Ibn Taymiyyah.**

**Ama kwa 4, Shaykh al-Fawzaan amesema ndani ya Ufafanuzi wa Twahaawiyyah nukta 200:**

**"Wao (Mashi'ah) kwa makosa wanasema kwamba 'Aliy ibn Abiy Twaalib**

**ambaye alitakiwa kuchukua Ukhaliyfah baada ya kifo cha Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam), na wanamwita 'Aliy wasii (mrithi aliyetajwa) wa Ummah huu. Nia ya Shi'ah ni kuleta matatizo tu na kuanzisha mitihani na mashaka baina ya watu." [Inapatikana yote kwa ukamilifu katika www.ittibaa.com]**

---

S9. Maswahaabah bora waliobakia ni *'asharah mubaasharah*. Ni kipi kinaweza kusemwa kuhusu *'aasharah mubaasharah*?

1. Wapo saba.
2. Wote wametajwa pamoja kwa majina na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) na kutueleza kwamba watapatiwa Pepo.
3. Hao ni wale tu Maswahaabah waliopewa bishara njema, wakati wakiwa hai, kwamba kwa hakika wataingia Peponi.
4. Walikuwa ni Makhaliyfah waliofaa.
5. Wote walikuwa ni mashahidi.
6. Wote walitoka katika [kabila la] Quraysh.
7. Wote walikuwa ni wanaume.

---

**Jibu: 2, 4, 6, 7.**

**Wao ni Maswahaabah kumi ambao walipewa bishara njema ya [kuingia] Peponi.**

**'Abdur-Rahmaan ibn 'Awf anasimulia kwamba Mjumbe wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema:**
"Abu Bakr yupo Peponi, 'Umar yupo Peponi, 'Uthmaan yupo Peponi, 'Aliy yupo Peponi, Twalhah yupo Peponi, Az-Zubayr yupo Peponi, 'Abdur-Rahmaan ibn 'Awf yupo Peponi, Sa'd ibn Abiy Waqqaas yupo Peponi, Sa'iyd ibn Zayd yupo Peponi, na Abu 'Ubaydah ibn al-Jarraah yupo Peponi."
**[Imesimuliwa na Ahmad na At-Tirmidhiy namba 4012. Shaykh Al-Albaaniy ameitangaza kuwa ni sahihi].**

**Ama kwa 3. Basi kuna idadi kubwa nyengine ya Maswahaabah ambao Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) ameeleza kwamba kwa uhakika wataingia Peponi. Miongoni mwao ni 'Ukkaashah bin Mihsan, kama ilivyo ndani ya Hadiyth iliyotajwa Sura ya 3 ya Kitaabut-Tawhiyd cha Muhammad ibn 'Abdil-Wahhaab.**

**Ama kwa 4, Imaam Al-Barbahariy ameeleza ndani ya Sharhus Sunnah**

**(Ufafanuzi wa *Iymaan*) nukta 28: "Wote wao walifaa kuwa ni Khaliyfah."**

S10. Waorodheshe Maswahaabah wafuatao kwa mtiririko wa ubora:

- Wale waliopigana katika vita vya Badr
- Wale walioukubali Uislamu baada ya mkataba wa Hudaybiyyah
- Wale waliofanya Hijrah mbili
- Wale waliokula kiapo cha utiifu chini ya mti (bayatur ridhwaan)

**Jibu:**

**Shayh Ahmad an-Najmiy amesema ndani ya ufafanuzi wake wa Sharhus-Sunnah cha Barbahariy (ukurasa 242):**

**"Nafasi ya *Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah* mbele ya Makhaliyfah watano kwa mtiririko wao – Abu Bakr, kisha 'Umar, kisha 'Uthmaan, kisha 'Aliy bin Abi Twaalib – kisha waliobakia katika kumi, kisha waliofanya H*ijrah* mbili, kisha yeyote aliyehamia kwenda al-MaDiynah, kisha Maswahaabah wa Badr, kisha Maswahaabah wa Baytur-Ridhwaan, kisha yeyote aliyeukubali Uislaam na kuhama kabla ya Kutekwa (yaani mkataba wa Hudaybiyyah), kisha waliokubali Uislamu baada ya Kutekwa, kisha wa chini kabisa katika Maswahaabah.."**

S11. Ni wepi bora zaidi, Muhajiruun au Answaar?

**Jibu: Muhajiruun.**

**Shaykh al-'Uthaymiyn anaeleza ndani ya kurasa zake kuhusu Al-'Aqiydah al-Waasitwiyyah (uk. 188): "Aina yao bora ni Muhajiruun kuliko Answaar kwa sababu Allaah ameendelea kuwataja Muhajiruun kuliko Answaar ndani ya Matamko Yake:** "Bila shaka Allaah Amewaelekea kwa rehma Mtume na Muhaajir na Answaar…" **[At-Tawbah: 117] Wao pia wamejumuisha kuhama kwao katika kuacha nyumba zao pamoja na mali na misaada yao.**

S12. Ni wepi kati ya wafuatao wametajwa kama ni tafsiri ya Swahaabah?

1. Kila mtu aliyesahibiana naye, iwapo ni kwa mwaka, mwezi, siku, saa,

au kwa kumuona [tu].
2. Yule ambaye amekutana na Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) akiwa na *Iymaan* naye, na kufariki akiwa ni Muislamu.
3. Yule ambaye ameishi katika wakati wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) na kufariki kama ni Muislamu.

**Jibu: 1 na 2.**

**Ama kwa 1, hii ni tafsiri iliyotolewa na Imaam Ahmad ndani ya 'Misingi Ya Sunnah'.**

**Ama kwa 2, hii ni ya Ibn Hajar iliyopo katika hadidu za chini za 'Misingi Ya Sunnah', ukurasa 8.**

**Ama kwa 3, basi ni mtu aliyeishi na alikuwa ni Muislamu katika wakati wa Mjumbe wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam), lakini hakumuona wala kukutana naye, na amefariki akiwa ni Muislamu, basi huyu anatambuliwa kuwa *Taabi'iyn Mukhadram*.**

**As-Sakhawiy amesema ndani ya Fat-hul Mughiyth (4/160):**

**Muhadhramuun (wale waliokubali Uislamu wakati wa Mjumbe wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) lakini hawakumuona) ni, kwa makubaliano ya wanachuoni wa Hadiyth, sio Maswahaabah. Isipokuwa wanahesabika kuwa ni miongoni mwa *Taabi'iyn* bora."**

S13. Ni wepi bora, Maswahaabah wa chini, au Taabi'uun walio bora kabisa (kizazi cha baada ya Maswahaabah)?

**Jibu: Maswahaabah wa chini.**
**Angalia nukta 46 ya 'Misingi Ya Sunnah'.**

**Wiki 7 Nukta 47-59**



## Maswali Kuhusu Watawala Waislamu

S1. Wepi kati ya wafuatao wanatambulika kuwa ni Amiyrul-Mu'miniin?

1. Mtu ambaye Ummah wa Waislamu unakubaliana naye.

2. Mtu ambaye amepigana katika nafasi ya utawala hadi kutambulika kuwa ni *Khaliyfah*.
3. Mtu ambaye asiyekuwa Muislamu.

---

**Jibu: 1 na 2.**

**Angalia nukta 47 na 48 za 'Misingi Ya Sunnah'.**

**Ama kwa 3, basi asiyekuwa Muislamu hawezi kutambulika kuwa ni *Amiyrul-Mu'miniyn*.**

---

S2. Majukumu yepi yafuatayo ni juu yake Mtawala Muislamu au mteuliwa wake?

1. Ni yule ambaye J*ihaad* inapiganwa kwa amri yake.
2. Mkusanyaji *Zakaah*.
3. Anafanyia kazi adhabu zilizowekwa.
4. Anatangaza siku ya 'Arafah, anasimama pamoja na mahujaji katika 'Arafah, na kuongozana nao Muzdalifah – hivyo wanamfuata katika sehemu kuu za *Hajj*.

---

**Jibu: zote hizo ni sahihi.**

**1, 2 na 3 zimetajwa na Imaam Ahmad ndani ya 'Misingi Ya Sunnah'.**

**Ama kwa 4, imetajwa ndani ya Maelezo ya Twahaawiyyah cha Shaykh Swaali al-Fawzaan, nukta 147.**

---

Allaah Anasema ndani ya Qur-aan:

"Mtiini Allaah na mtiini Mtume na wenye mamlaka juu yenu." [An-Nisaa: 59]

S3. Iwapo mtawala Muislamu atatuamuru dhambi, Je, tuitii amri hii?

1. Ndio
2. Hapana

---

**Jibu: Hapana. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam)**

**amesema:** “Kumsikiliza na kumtii ni (lazima) juu ya Muislamu katika analolipenda na asilolipenda, alimradi tu haamrishwi katika dhambi. Iwapo ataamrishwa katika dhambi, basi hakuna kusikiliza wala kutii.” **[Al-Bukhaariy na Muslim].**

S4. Katika Hadiyth ya Hudhayfah ibn al-Yamaan, Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa aalihi wa sallam) ametuambia kuwatii watawala, hata kama watakuwa na sifa zisizoelekea. Ni sifa zipi zifuatazo amezitaja?

1. Wana mioyo ya kishetani na miili ya binaadamu.
2. Wanaacha *Swalah*.
3. Wanachapa mgongo wako.
4. Wanatenda shirk kubwa.
5. Hawafuati muongozo wa Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa aalihi wa sallam) wala *Sunnah* yake.
6. Wanachukua mali yako.

**Jibu: 1, 3, 5, 6.**

**Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa aalihi wa sallam) amesema ndani ya Hadiyth ya Hudhayfah:** Kutakuja viongozi ambao hawatafuata muongozo wangu na wala hawatafuata *Sunnah* yangu. Kutakuwa na watu miongoni mwao ambao watakuwa na mioyo ya kishetani ndani ya miili ya binaadamu. **Hudhayfah akauliza: Je, nifanye nini ewe Mtume wa Allaah iwapo nitafikia katika (hali) hiyo? Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa aalihi wa sallam) akajibu:**
Umsikilize na kumtii mtawala wako hata kama iwapo atakuchapa mgongo wako na kuchukua mali yako, basi endelea kumsikiliza na kumtii. **[Hadiyth imesimuliwa na Muslim (3/1029/4554)].**

S5. Mtawala Muislamu anaweza kutumbukia katika dhambi (ndogo zaidi kuliko ile ambayo itamtoa katika Uislamu kwa pamoja). Kwa sababu ya hili, baadhi ya watu wanaweza kuacha kuswali nyuma yake. Ni zipi baadhi ya athari ya hili?

1. Kuvunja nyadhifa za Waislamu.
2. Kugawa umoja wa Waislamu.
3. Kumwaga damu.

4. Umoja wa idadi ya watu Waislamu [kusambaratika].

**Jibu: 1, 2 na 3. Angalia Shaykh al-Fawzaan katika Ufafanuzi wa al-'Aqiydah at-Twahaawiyyah nukta 152: '... na katika kuacha *Swalah* nyuma yake kuna athari nyingi mbaya. Athari zake zinaanza kwa kuvunja nyadhifa za Waislamu, kugawa umoja wao na kumwaga damu zao. Kwa hivyo katika hili lizuiliwe.'**

**Ama kwa 4, kuacha kuswali nyuma ya Mtawala Muislamu muovu kunapelekea mfarakano na sio mjumuikano.**

S6. Je, tufanyeje iwapo tutafanya *Hajj* pamoja na mtawala Muislamu na kumuona akinywa pombe huku akifanya *Hajj*?

1. Kuendelea kutekeleza *Hajj* pamoja naye, hali ya kuwa tunachukia dhambi hiyo anayoifanya.
2. Kuchapisha na kueneza vipeperushi vinavyoeleza kosa la mtawala, katika matarajio ya kwamba hili litamfanya kuacha kunywa pombe katika siku za mbele na kumhamasisha kuomba tawbah kwa Allaah, Mtukufu.
3. Kuacha kufanya *Hajj* haraka iwezekanavyo.

**Jibu: 1. Shaykh al-'Uthaymiyn anaeleza ndani ya ufafanuzi wake wa al-'Aqiydah al-Waasitwiyyah:**

**Mawazo yao wao (Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah) katika kufanya *Hijjah* pamoja na watawala (Muislamu) kama ni jambo sahihi, hata kama (watawala) ni waovu – hata kama wao (watawala) wanakunywa pombe wakati wa *Hijjah*.**

**Wao (Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah) hawasemi: 'Huyu ni mtawala muovu, na hatukubali uongozi wake'. Hii ni kwa sababu mawazo ya (Ahlus-Sunnah wal-Jamaa'ah) katika kumtii kiongozi wa Waislamu ni jambo ambalo ni la lazima, hata kama yeye ni muovu – kwa sharti la kwamba uovu wake hauendi katika hali inayoonesha wazi kufru ambayo itakuwa ni ushahidi kwetu mbele ya Allaah.**

S7. Ni wakati gani tuache kufanya J*ihaad* pamoja na watawala Waislamu ambao ni waovu (wakiwa na madhambi ambayo ni madogo yasiyomtoa mtu nje ya Uislaam)?

1. Hata siku moja, hadi Qiyaamah.
2. Pale 'Iysaa ibn Maryam atakaposhuka kabla ya mwisho wa wakati.
3. Pale watawala watakapoacha matakwa ya idadi kubwa ya Waislamu.

---

**Jibu: 1.**

**Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amewaambia Answaar:** "Kuweni na subra hadi mkutane na hawdh (hodhi)." **[Imesimuliwa na al-Bukhaariy. Angalia suala la 9 kuona ni kwa nini Hadiyth hii inaweza kutumiwa katika maelezo haya].**

**Ama kwa nukta 3, basi hili ni jambo ambalo linafanana na demokrasia, suala ambalo linakatazwa ndani ya Uislamu.**

---

S8. Iwapo mmoja wetu atamuona mtawala Muislamu akifanya jambo lisilo sahihi, ni kwa njia gani tulichukulie hilo?

1. Kumchukua katika mikono
2. Kumwambia kwa ufaragha
3. Kuwatahadharisha watu wa Ummah kuhusiana na dhambi alizotenda hadharani
4. Kuacha kumuombea dua'a

---

**Jibu: 1 na 2.**

**Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema:** "Yeyote anayependelea kumshauri mtu aliyekuwa na uongozi basi na asifanye hadharani, isipokuwa amchukue mkononi na kumchukua sehemu tofauti (na kumshauri). Na iwapo atakubali (ushauri huo) kutoka kwake basi (amefanikiwa lengo lake) na iwapo sivyo, basi amefanikiwa lile ambalo lilikuwa ni jukumu juu yake." **[Ahmad 3/403 na ibn Abiy 'Aaswim 2/521].**

**Mtu mmoja alimuuliza Shaykh Bin Baaz: "Ni kwa nini huwashauri watawala wa Waislamu?" Hivyo Shaykh mtiifu akamjibu: "Ni nani aliyekwambia kwamba sifanyi hivyo?"**

**Rejeo hizi zimechukuliwa kutoka Uwekaji Wazi wa Hali Halisi ya Mambo, ukurasa 29.**

---

S9. Ni lipi linaweza kusemwa kuhusu Muislamu anayepingana (kivita) dhidi ya mtawala Muislamu hata kama iwapo mtawala huyo anatenda madhambi (ambayo ni ya chini yasiyomtoa nje ya Uislamu)?

1. Yeye ni mmoja miongoni mwa Khawaarij.
2. Amesababisha mgongano miongoni mwa Waislamu.
3. Amefanya jambo zuri, kwa kujaribu kuleta mabadiliko ya Ummah wa Waislamu (taifa).
4. Amefanya jambo ambalo ni kinyume na mafundisho ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) na Salaf.
5. Anafariki katika kifo cha *jaahiliyyah* (Ujinga wa Kabla ya Uislamu).

---

**Jibu: 1, 2, 4 na 5.**

**Imaam al-Barbahaariy amesema: 'Yeyote anayepingana kivita dhidi ya mtawala Muislamu ni miongoni mwa Khawaarij, amesababisha fitna ndani ya Waislamu na amekwenda kinyume na mapokezi na anafariki kifo cha siku za *jaahiliyyah*. Hairuhusiki kupigana na mtawala wala kuanzisha vita (msituni) dhidi yake hata kama iwapo yeye ni mdhalilishaji. Hii ni kwa sababu ya matamko ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) kwa Abu Dharr al-Ghifaariy: "Kuwa na subra hata kama yeye ni mtumwa wa Kihabeshi," na matamko yake (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) kwa Answaar:** "Kuwa na subra hadi utakapokutana na mimi katika Hawdh." **Hakuna kupigana dhidi ya mtawala ndani ya *Sunnah*. Inasababisha uvunjifu wa Diyn na Maswali ya dunia." Ufafanuzi wa *Iymaan*, nukta 33 na 34.**

**Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema ndani ya *Hadiyth* ya ibn 'Abbaas:** Anayeona kutoka kwa mtawala wake kitu ambacho hakipendi, muache awe na subra naye, kwani yule anayesababisha mfarakano kutoka kwa *Jamaa'ah* kwa kipande cha mkono [wake] na kufariki, basi amefariki kifo cha *Jaahiliyyah*. **[Hadiyth imesimuliwa na al-Bukhaariy (9/145) na Muslim na wengineo].**

---

S10. Ni adhabu gani ambayo watawala Waislamu walimuadhibu Imaam Ahmad ibn Hanbal, ambayo kwayo akaruhusu wanafunzi wake na wafuasi wake kupigana vita dhidi yao?

1. Baada ya kuchapwa bakora zilizosababisha kukosa hisia (kulemaa mwili).
2. Baada ya maadui wapotofu wa *Sunnah*, ibn Abiy Duwaad, kusema kwamba Imaam Ahmad alikuwa ni mpotofu na kuchapwa bakora kuendelea.
3. Hapana.

**Jibu: 3. Al-Khallal amesimulia ndani ya As-Sunnah (namba 87) kwamba Abu Bakr alitusimulia akisema:**

**Nimemsikia Abu 'Abdillaah (Imaam Ahmad) akiamuru kwamba umwagaji damu usitekelezwe na kwa mkazo akikataza kuacha vita. Angalia hadudi za chini, nukta 34 ya Ufafanuzi wa *Iymaan* (tafsiri ya Kiingereza).**

S11. Ni aina gani ya upiganaji vita ambao Waislamu wanafanya dhidi ya mtawala Muislamu pale anapotumia unyanyasaji wa kimwili (kwa mfano kupigana) dhidi ya Waislamu na kuiba mali zao?

1. Wanamfuata kiongozi wa Jeshi la Waislamu ndani ya nchi hiyo wakiomba kumuondosha mtawala huyo.
2. Hawatafanya vita dhidi ya mtawala huyu, alimradi tu yeye anabaki kuwa ni Muislamu.
3. Wanapigana naye vita kwa njia ya kalamu – yaani kwa kuandika vitabu na vipeperushi wakihamasisha watu kumuondosha mtawala wao.

**Jibu: 2**

**Angalia Hadiyth ya Hudhayfah bin al-Yamaan iliyoelezewa hapo kabla.**

S12. Ni kiongozi yupi wa Waislamu aliuliwa na baadhi ya Maswahaabah wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam)?

1. Mu'aawiyah ibn Abiy Sufyaan.
2. Al-Hajjaaj ibn Yuusuf.
3. Marwaan ibn al-Hakam.

**Jibu: 2. Yeye ni ath-Thaqafiy na anatambulikana sana. Adh-Dhahabiy amesema ndani ya Siyaar A'laam in-Nubalaa (4/343) mwisho mwa wasifu wake: "Tunapingana naye na wala hatumpendi, isipokuwa ni kwamba tunamchukia kwa ajili ya Allaah. Alikuwa na matendo mema, lakini**

**yamezama baharini kwa madhambi yake, na kadhia yake ipo kwa Allaah." Rejeo imechukuliwa kutoka Ufafanuzi na Uwekaji Wazi wa Hali Halisi ya Mambo, ukurasa 30 kama ni hadidu za chini.**

**Angalia 'Misingi Ya Sunnah', hadidu za chini, ukurasa 141.**

S13. Ni Maswahaabah gani wafuatao walipigana dhidi yake?

1. Ibn 'Umar
2. Anas
3. Abu Bakr
4. Hakuna hata mmoja

**Jibu: Hakuna hata mmoja.**

**Ibn 'Umar na Anas walimuombea dua'a nyuma yake, kama ilivyotajwa na Shaykh Bin Baaz ndani ya Fataawa Islaamiyyah, juzuu 1, ukurasa 158.**

**Ama kwa Abu Bakr, hii ilikuwa ni miaka kadhaa baada ya yeye kufariki.**

S14. Kulikuwa na athari gani pale kundi la watu lilipopigana vita dhidi ya Hajjaaj katika jaribio la kuzuia udhalilishaji wake?

1. Walizuia udhalilishaji wake.
2. Walipunguza udhalilifu wa Waislamu chini ya utawala wake.
3. Wote waliuliwa, na hakuna zuri lolote lililoletwa na wao.

**Jibu: 3**

**Imesimuliwa na Ibn Sa'd ndani ya Tabaqaatul Kubraa (7/163-165): Kundi la Waislamu lilimjia al-Hasan al-Basriy (110 AH) likiomba fatwa kuhusu kupigana vita dhidi ya al-Hajjaaj. Hivyo wakasema: 'Ewe Abu Sa'iyd! Unasemaje kuhusu kumpiga vita mdhalilishaji huyu ambaye bila halali ameeneza damu na bila ya halali amechukua mali na hili na lile?' hivyo al-Hasan akasema: 'Ninahukumu kwamba asipigwe vita. Iwapo hii ni adhabu kutoka kwa Allaah basi hamtaweza kuiondosha kwa mapanga yenu. Iwapo huu ni mtihani kutoka kwa Allaah basi kuweni watulivu hadi hukmu ya Allaah itakapokuja, na Yeye ni mbora wa Mahakimu.' Hivyo wakamuacha al-Hasan, wakiwa hawajakubaliana naye na kupigana dhidi yake al-Hajjaaj – hivyo al-Hajjaaj akawaua wote. Kuhusu hao wapiganaji, al-Hasan alikuwa akisema: 'Iwapo watu wangekuwa na subra pale wanapojaribiwa**

**kwa mtawala wao mdhalilishaji, haitakuwa ni muda mrefu hadi pale Allaah atakapowapatia njia ya kutokea. Hata hivyo, wanakimbilia mapanga yao, kwa hivyo wameachiwa mapanga yao. Naapa kwa Allaah! Hakuna siku hata moja walioleta zuri lolote.'**

S15. Je, neno Khawaarij linaweza kutumika kwa wale wanaopigana dhidi ya mtawala Muislamu?

1. Ndio
2. Hapana

**Jibu: 1.**

**Imaam al-Barbhaariy amesema: 'Yeyote anayepigana dhidi ya mtawala Muislamu ni mmoja miongoni mwa Khawaarij, amesababisha mfarakano baina ya Waislamu na amekwenda kinyume na mapokezi na anakufa kifo cha siku za *Jaahiliyyah*.' Ufafanuzi wa *Iymaan*, nukta 33.**

S16. Maneno yepi yafuatayo ni kweli kuhusu Khawaarij?

1. Wao ni majibwa ya Motoni.
2. Wanapita katika dini kama vile mshale.
3. Wapo miongoni mwao wanaoswali na kufunga kwa sana kabisa.

**Jibu: zote hizo.**

**Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema:** "Khawaarij ni majibwa ya Motoni." **[Ahmad, swahiyh]**

**Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema:** "Kundi litapita linalosoma Qur-aan, haitavuka shingo zao, kila wakati kundi likipita linakata, hadi Dajjaal atakapodhihiri pamoja nao." **[Ibn Maajah].**

S17. Ni watu wepi wafuatao wametoa matamshi ya wazi wazi kuhusiana na msimamo wa Khawaarij, kwa ushahidi wa maandishi yao na maelezo yao ya wazi?

1. Usaamah bin Ladin
2. Hasan al-Bannah, muanzilishi wa Ikhwaanul Muslimuun
3. Mawdudi, mmoja miongoni wa viongozi wa Ikhwaanul Muslimuun
4. Hasan at-Turaabi, mmoja miongoni mwa viongozi wa Ikhwaanul Muslimuun nchini Sudan
5. Sayyid Qutb, muanzilishi wa Ikhwaanul Muslimuun

**Jibu: Wote hao.**

S18. Iwapo kama hakuna *Amiyrul-Mu'miniyn*, basi ni njia gani sahihi ya kumleta *Amiyrul-Mu'miniyn*?

1. Kuusafisha Ummah wa Waislamu na kuwatoharisha katika *'Aqiydah* sahihi na M*anhaj* (tasfiyyah na tarbiyyah)
2. Kumchagua mmoja
3. Kuwakusanya watu katika makundi ya Waislamu wakiwa na mabango, wakiacha kufuata *'Aqiydah* na M*anhaj*
4. Kushirikiana na wote ambao wanaopendelea katika kuleta amiyr, bila ya kujali wanatoka kutoka kundi gani la Waislamu

**Jibu 1: Njia nyengine zilizotajwa haziruhusiki.**

**Shaykh Al-Albaaniy (Rahimahu Allaah) ameongeza kuhusiana na nukta 157 na 158 ya Twahaawiyyah:**

**'Mfafanuzi ibn 'Abil 'Izz ametaja *Ahaadiyth* nyingi kuhusiana na hili ambazo unaziona zimetajwa ndani ya kitabu chake.**

**Ibn Abil 'Izz amesema:**

**Ama kwa kushikana na kuwatii hata kama ni wadhalilishaji, basi hii ni kwa sababu ya maovu ambayo yamezalishwa kwa kupigana vita dhidi yake, maovu haya yakiwa ni ya muda mrefu zaidi kuliko udhalilishaji wao unaweza kuzalisha. Kwa hakika, kuwa na *Iymaan* juu ya wadhalilishaji unaondosha madhambi kwa sababu Allaah hakumpatia uongozi juu yetu isipokuwa kwa sababu ya ufisadi wa matendo yetu na malipo kufuata kwa mujibu wa aina ya tendo. Hivyo kilichokuwa wajibu juu yetu ni kushikana katika *Istighfaar* (kuomba msamaha kwa Allaah) na kuomba *tawbah* (kutubia) na kurekebisha matendo yetu.**

**Yeye, Mtukufu, Amesema:**

"Na malipo ya ubaya ni ubaya ulio sawa na (ubaya) huo; lakini anayesamehe na kusuluhisha ugomvi; ujira wake uko kwa Allaah, bila shaka hawapendi madhaalim." **[Ash-Shuwraa: 30]**

**Vivyo hivyo, tunawaweka wadhalilishaji katika uongozi dhidi ya wengine kwa sababu ya matendo waliyoyachuma:**

"Na vivi hivi Tunawatia mapenzi baadhi ya madhalimu juu ya wengine (wakapiganiana) kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma (kwa pamoja)." **[Al-An'aam: 129]**

**Hivyo watu (chini ya mtawala) wanataka kujiachia huru kutokana na udhalilishaji wa mtawala, basi na waache udhalilishaji.**
**[mwisho wa maneno ya Ibn Abil 'Izz. Shaykh al-Albaaniy anaendelea]**

**Ninasema: hili lina maelezo ya njia ya nyinyi kujiachia huru kutoka kwa watawala wadhalilishaji, wale waliokuwa na ngozi zetu na kuzungumza kwa ndimi zetu – na ndio ilivyo: kwamba Waislamu wanaomba *tawbah* kwa Mola wao na kusahihisha *Iymaan* zao, na kuleta kwa mikono yao na familia zao juu ya Uislamu ulio sahihi, wakielewa Maneno Yake, Mtukufu:**

"Hakika Allaah habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo katika nafsi zao." **[Ar-Ra'ad: 11]**

**Na hili limeoneshwa na mmoja wa walinganiaji waliopo enzi za leo akisema: 'Simamisha taifa la Uislamu ndani ya nyoyo zenu, itasimamishwa kwa ajili yenu juu ya ardhi zenu.'**

**Na njia ya kujiachia huru kwetu wenyewe (yaani kutokana na watawala wadhalilishaji) sio kama watu wanavyofikiria, kwamba ni kwa mapinduzi ya vita dhidi ya watawala, kwa njia ya majeshi ya nguvu, kwani hili – pamoja na ukweli kwamba ni uzushi wa siku za leo – basi pia ni kinyume na maandiko ya *Shari'ah*; kutoka kwao kuwa na amri ya kusahihisha yale yaliyomo ndani yetu.**

**Hivyo ni lazima kusahihisha msingi ili kujenga Jengo juu yake.**

"Na bila shaka Allaah humsaidia yule anayesaidia Diyn Yake. Hakika Allaah ni Mwenye nguvu na Mwenye kushinda." **[Al-Hajj: 40]**

S19. Je, inaweza kusemwa vipi kuhusiana na kufanya dua'a kwa mtawala Muislamu?

1. Ni njia ya kuonesha utiifu kwake.
2. Kufanya dua'a dhidi yake, kwa ukweli, ni kupigana vita dhidi yake.
3. Ni muhimu kufanya dua'a.

**Jibu: Zote hizo.**

**Shaykh Swaalih al-Fawzaan aliulizwa kuhusu namna ya kuonesha utiifu kwa mtawala Muislamu kwa mujibu wa Shari'ah. Alijibu:**

**Utiifu kwa watawala unajumuisha yafuatayo: Kufanya dua'a kwa yaliyo sahihi na ukakamavu wao, kwani ni kutokana na *Sunnah* kufanya dua'a kwa watawala Waislamu, haswa kipindi ambacho dua'a hukubaliwa na sehemu ambazo inaaminiwa kwamba dua'ah hujibiwa.**

**Al-Fudhwayl ibn ´Iyaadhw amesema: "Iwapo nitakuwa na dua'a ambayo itajibiwa nitamuombea dua'a mtawala." Hii ni kwa sababu ya kubadilika kwa mtawala kunaathiri kubadilika kwa jamii, na kunapokuwa na ufisadi kwa mtawala kutakuwa na ufisadi kwa jamii.**

**Na kwa utiifu mbele ya watawala ni kutekeleza majukumu waliyoteuwa kwa waajiriwa. Na miongoni mwa utiifu mbele yao ni kuwaelezea makosa na maovu yao yanayotokezea ndani ya jamii, pale wanapokuwa hawayatambui. Hata hivyo, hili lifanyike kwa faragha baina ya yule anayeshauri na wao [watawala]. Sio ushauri unaotolewa mbele ya hadhara ya watu au mjumuiko, kwa sababu hili linaleta uadui baina ya watawala na watawaliwa.**

**Sio ushauri mzuri kwamba mtu azungumzie makosa ya watawala juu ya mjumuiko au juu ya kiti mbele ya watu, hili halitasaidia, isipokuwa kuengeza uovu zaidi na zaidi. Ushauri mzuri ni kwamba umuelekee mtawala kibinafsi kwa maandishi au njia ya wale wanaoweza kuwasiliana nao na kufikisha ushauri wao kwa faragha baina yao na wao. Na pia sio ushauri mzuri kwamba tunaandika katika kuwapinga na kuyatawanya miongoni mwa watu na kusema kwamba hii ni miongoni mwa ushauri mzuri. Hapana! Hii ni kuwaripua (kwa makosa yao) na kwa yale mambo yanayosababisha maovu, na maadui, na ni watu wa utashi ambao wanaingia katika mambo na njia hizi.**

**Ama kwa 2, Shaykh al-Fawzaan amesema: "Kufanya dua'a dhidi ya watawala Waislamu inaangukia chini ya maana ya khuruuj (kufanya vita) dhidi yao – kama ilivyo kufanya vita dhidi yao kwa zana za vita.**

**Na mtu anayeomba dua'a dhidi ya watawala anatokezea kwa sababu hakubaliani kwamba wao ni watawala sahihi.**

**Ama kwa 3, angalia maneno ya al-Fudhwayl yaliyonukuliwa hapo juu.**

## Wiki 8 Nukta 60-68



### Maswali Kuhusu Nani Anayekwenda Peponi na Motoni

S1. Iwapo mtu fulani atakufa, hatusemi kwa uhakika kwamba atakwenda Peponi au Motoni. Hata hivyo, ni matamshi yepi yafuatayo ni sahihi kusema?

1. "Waumini watakuwa Peponi, na wasioamini watakuwa Motoni."
2. "Mtu yeyote ambaye Allaah au Mtume Wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) wametueleza kwamba atakuwa Peponi au Motoni basi atakuwemo humo."
3. "Binti wa Mfalme Diana alifariki kama asiyekuwa Muislamu, hakuna shaka yoyote kwamba atakwenda Motoni."
4. "Ami yangu amefariki kama Muislamu, hivyo kwa uhakika ataingia Peponi."

---

**Jibu: 1 na 2**

**Angalia nukta 60 ya 'Misingi Ya Sunnah' na hadidu zake za chini.**

---

S2. Ni watu gani wafuatao ametueleza Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) kwamba wataingia Peponi?

1. 'Abdur-Rahmaan ibn 'Awf
2. Ukkaashah ibn Mihsaan
3. Bilaal
4. 'Abdullaah bin Salaam
5. Khadiyjah
6. Az-Zubayr ibn al-'Awwaam

---

**Jibu: Wote hao.**

**Baadhi ya watu ambao Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amethibitisha kuingia Peponi ni:**

- **Watu kumi walioahidiwa Pepo (angalia Hadiyth iliyotajwa kipindi**

**cha wiki ya 6) Unaweza kukumbuka ni kina nani?**

- **Ukkaashah ibn Mihsaan, ambaye alimuuliza Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) kumuombea dua'a kwamba atakuwa miongoni mwa watu alfu sabiini watakaoingia Peponi bila ya kuhesabiwa, kama ilivyotajwa ndani ya Surah ya 3 ya Kitaabut-Tawhiyd cha Muhammad ibn `Abdil-Wahhaab**
- **Bilaal, ambaye nyayo zake Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amezisikia Peponi katika usiku wa Mi'raaj**
- **Abdullaah bin Salaam, ambaye Sa'd ibn Abiy Waqqaas amesema:** "Sikupata kumsikia Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) akisema kuhusu mtu yeyote kutembea juu ya ardhi kwamba ni miongoni mwa watu wa Peponi isipokuwa ni Abdullaah ibn Salaam..." **[Imepokewa na Al-Bukhaariy ndani ya swahiyh yake]**
- **Khadiyjah, ambaye Jibriyl amemueleza Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) kufikisha salamu kwake kutoka kwa Mola wake, na kutoka kwake mwenyewe, na bishara njema ya makaazi ya Peponi yaliyotengenezwa kwa lulu tukufu, ambamo hakutakuwa na kelele wala uchofu. Imepokewa na Al-Bukhaariy ndani ya swahiyh yake**

S3. Ni watu gani wafuatao tumeelezwa kwamba wataadhibiwa ndani ya Moto?

1. Fir'awn
2. Watu wa Fir'awn
3. Abu Lahab
4. Mke wa Abu Lahab
5. Al-Waliyd ibn al-Mughiyrah al-Makhzuum

**Jibu: Wote hao.**

**Ama kwa Fir'awn na watu wake, wametajwa ndani ya Suuratul-Muuminiyn:**

"Adhabu za Motoni wanadhihirishiwa (makaburini mwao) asubuhi na jioni. Na siku ile kitakapotokea Qiyaamah (kutasemwa): 'Waingizeni watu wa Fir'awn katika adhabu kali zaidi (kuliko hii waliyoipata kaburini).' " **[Al-Mu'miniyn: 46]**

**Ama kwa Abu Lahab na mkewe, wametajwa ndani ya Suuratul-Masad.**

**Ama kwa Al-Walliyd ibn al-Mughiyrah al-Makhzuumi, ametajwa ndani ya Suuratul-Muddaththir:** "Karibuni hivi Nitamtia katika Moto (unaowaka kweli kweli)." **[Al-Muddaththir: 26]**

S4. Ni yepi yafuatayo yanawezakana kutokea kwa muumini?

1. Ataingia Peponi moja kwa moja bila ya kuadhibiwa.
2. Ataingia Motoni na atabakia humo milele.
3. Ataingia Motoni na kuadhibiwa kwa muda kisha atatolewa na kuingia Peponi milele.

**Jibu: 1 na 3**

**Ama kwa 1, inajulikana kwa umaarufu kabisa.**

**Ama kwa 2, Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema:** "Yeyote atakayekutana na Allaah, akiwa hajamshirikia na chochote kama mshirika pamoja naye, ataingia Peponi. Na yeyote atakayekutana naye, akiwa amemshirikisha na kitu kama ni mshirika pamoja naye, ataingia Motoni." **[Hadiyth imepokewa na Muslim].**

**Ama kwa 3, Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema:** "Ama kwa watu wa Motoni ambao wanahusika nao, wataishi humo milele, bila ya kufa wala kuishi. Lakini kuna watu ambao Moto utawaunguza kwa sababu ya madhambi yao na kuwasababishia kufa. Baada ya kubadilika na kuwa ni makaa yaliyokufa. Ruhusa itatolewa kwa kuombewa shafaa'ah, na wataletwa kwa makundi na kutawanywa kupitia mito ya Peponi. Watu wa Peponi wataambiwa: 'Wamiminieni maji juu yao.' Hivyo, wataota kama vile mbegu zinapopigwa na maji ya mvua." **[Hadiyth imepokewa na Muslim].**

S5. Ni yepi yafuatayo yanawezekana kutokea kwa mtu asiyeamini na aliyekana Uislamu ulipokuja kwake ndani ya dunia hii?

1. Ataingia Peponi moja kwa moja bila ya kuadhibiwa.
2. Ataingia Motoni na kubakia humo milele.
3. Ataingia Motoni na kuadhibiwa kwa muda kisha atatolewa nje na kuingizwa Peponi milele.

**Jibu: namba 2 tu.**

**Allaa Anasema ndani ya Qur-aan:**

“Hakika waliokufuru na wakafa hali ni makafiri, hao iko juu yao laana ya Allaah na ya Malaaikah na ya watu wote. Humo (kwenye adhabu ya laana-Motoni) watakaa daima. Hawatapunguziwa adhabu wala hawatapewa muda wa kupumzika.” **[Al-Baqarah: 161-162]**

S6. Je, mtenda madhambi makubwa ataingia Peponi?

1. Hapana, haiwezekani.
2. Ndio, baada ya kukaa muda ndani ya Moto.
3. Ndio anaweza kuingia Peponi bila ya kuingia Motoni.

**Jibu: Hili linahitaji maelezo.**

**Ama kwa jibu namba 1, hii ni kwa ajili tu ya watenda madhambi makubwa ambao hawajaamini – yule ambaye anaamini kwamba dhambi hiyo inaruhusiwa. Wasioamini kamwe hawataingia Peponi.**

**Ama kwa jibu namba 2 na namba 3, mtenda madhambi makubwa ambaye ni muumini ataingia Peponi, na inawezekana au haitowezekana kuadhibiwa kabla ya kuingia kwake Peponi, kama ilivyofafanuliwa na Shaykh Swaali al-Fawzaan:**

**“Ama kwa dhambi ambayo sio kufr wala shirk ambayo itamtoa mtu nje ya Diyn, basi hatutangazi [kwamba huyo Muislamu] ni mtu asiyeamini kwa sababu ya hilo. Isipokuwa, tunashikilia msimamo wa *‘Aqiydah* yetu kwamba yeye ni muumini mwenye kasoro katika *Iymaan* yake, chini ya hofu [ya adhabu] na chini ya Matakwa na Uwezo wa Allaah. Hii ndio *‘Aqiydah* ya Muislamu alimradi tu hatangazi hilo (dhambi yake) kuwa ni uhakika kwamba ni halaal (inaruhusiwa).” Ufafanuzi wa Twahaawiyyah, nukta 131.**

S7. Dhambi gani ambayo Allaah Anasamehe?

1. Atasamehe dhambi yoyote ambayo imeombewa *tawbah*.
2. Atasamehe dhambi yoyote ambayo imeombewa *tawbah* isipokuwa kwa

shirk.

3. Anaweza kusamehe dhambi yoyote ya muumini ikiwemo shirk, hata kama hajaiombea tawbah, Akipenda.
4. Anaweza kusamehe dhambi yoyote iliyotendwa na muumini, kama Akipenda – dhambi yoyote, isipokuwa kwa shirk ambayo mtu atakufia nayo bila ya kuiombea *tawbah*.

---

**Jibu: 1 na 4.**

**Ama kwa 1 na 2, Allaah Anasema ndani ya Qur-aan:**

"Sema: "Enyi waja Wangu mliojidhulumu nafsi zenu! Msikate tamaa na rahmah ya Allaah; bila shaka Allaah husamehe dhambi zote; hakika Yeye ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu." **[Az-Zumar: 53]**

**Ama kwa 3, angalia nukuu ya Swaalih al-Fawzaan katika suala lililopita.**

**Ama kwa 4, Allaah Anasema ndani ya Qur-aan:**

"Hakika Allaah hasamehe kushirikishwa; na Husamehe yasiyokuwa haya kwa Amtakaye. Na anayemshirikisha Allaah bila shaka amebuni dhambi kubwa." **[An-Nisaa: 48]**

---

S8. Angalia mchoro uliopo hapo chini.

Muislamu anatenda dhambi kubwa

Dhambi hiyo imeelezewa adhabu yake kwa mtawala Muislamu | Dhambi haijaeelezewa adhabu yake kwa mtawala Muislamu

adhabu inatolewa | adhabu haitolewi | mtenda dhambi anatubia | mtenda dhambi hatubii

A | B | C | D

Ni hali zipi mbili kati ya nne (A, B, C au D) zitakazomuachia huru Muislamu kutokana na hatari ya adhabu ya Allaah siku ya Qiyaamah kwa dhambi kubwa ambayo ameitenda?

---

**Jibu: A na C.**

**Angalia 'Misingi Ya Sunnah' nukta 62 na 63.**

9. Linganisha baina ya kundi potofu na *Iymaan* yake potofu kuhusiana na mada hii.

| | |
|---|---|
| Khawaarij | Mtenda dhambi kuu ndani ya maisha haya hatambuliwi kuwa ni muumini wala kafiri. |
| Mu'tazilah | Mtenda dhambi kuu ni muumini mwenye I*ymaan* kamili. |
| Murji-ah | Mtenda dhambi kuu ndani ya maisha haya ni mtu asiyeamini (kafiri).<br>Hapo siku ya Qiyaamah atakuwa ndani ya Moto |

**Jibu:**

**Khawaarij: Mtenda dhambi kuu ndani ya maisha haya ni mtu asiyeamini (kafiri).**
**Hapo siku ya Qiyaamah atakuwa ndani ya Moto milele.**

**Mu'tazilah: Mtenda dhambi kuu ndani ya maisha haya hatambuliwi kuwa ni muumini wala kafiri.**

**Murji-ah: Mtenda dhambi kuu ni muumini mwenye *Iymaan* kamili.**

S10. Ni watu gani wafuatao anayemtambua Imaam Ahmad kuwa ni mzushi?

1. Mtu ambaye anayezungumzia vibaya na kumshusha hadhi *Swahaabah* mmoja.
2. Mtu ambaye asiyempenda *Swahaabah* mmoja.
3. Mtu ambaye anayetaja udhaifu wa *Swahaabah*.

**Jibu: zote hizo. Angalia nukta 67 ya 'Misingi Ya Sunnah'.**

S11. Dua'a ifuafayo mara nyingi hutajwa ndani ya mfumo wa kuwaombea dua'a Maswahaabah. Ni maneno gani mawili yamepungua?

"Mola wetu! Tusamehe sisi na ndugu zetu waliotutangulia (kufa) katika ______A_____. Wala usijaaliye katika nyoyo zetu ______B_____ kuwafanyia Waislamu (wenzetu).}" **[Al-Hashr: 10]**

**Jibu: A=*iymaan* (imani) B= *ghill* (undani/uchoyo/ugomvi)**

S1. Je, inawezekana kwa mtu kuwa na sifa za unafiki na *Iymaan* kwa wakati mmoja.

---

**Jibu: Ndio**

**Shaykh Swaalih al-Fawzaan amesema ndani ya kitabu chake: Kitabu cha Tawhiyd/'Aqiydah Tawhiyd:**

**Unafiki ni wa aina mbili:**

**Aina ya kwanza: Unafiki unauhusisha *Iymaan*, ambao ni *nifaaq akbar* (unafiki mkuu) - unafiki mkubwa. Mtu anayetumbukia ndani ya (aina hii) kwa nje anauonesha Uislamu lakini ndani anaficha ukafiri. Aina hii (ya unafiki) inamtoa mtu nje ya Diyn, na mtu anayetumbukia ndani yake atakuwa sehemu ya chini kabisa ya Moto...**

**Na (watu) hawa wapo kila enzi, haswa pale nguvu za Uislamu zinapojitokeza, na wao (wanafiki) hawawezi kupigana dhidi ya muonekano wao wa nje – hivyo wanaonesha muonekano wao nje kwamba wameingia ndani yake (Uislamu) ili kufanya hujma dhidi yake na watu wake kiundani – na hivyo wanaweza kuishi maisha marefu pamoja na Waislamu na kuifanya damu yao na mali yao kutopigwa vita.**

**Aina ya pili: Unafiki wa kitendo; na hii ni kufanya kitendo kutoka kwenye matendo ya wanafiki, huku akiwa bado na *Iymaan* ndani ya moyo. Hii (aina) haimtoi mtu nje ya Diyn, lakini ni njia ya kumfikisha huko. Mtu mwenye msimamo huu anachangana I*ymaan* na unafiki. Kisha huyo (mnafiki) anaonekana zaidi, anakuwa safi kabisa mnafiki asiyejiharibu. Ushahidi wa hili ni maneno ya Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam):**

"Alama za mnafiki ni nne – yeyote mwenye nazo zote ni mnafiki safi asiyejiharibu, na yeyote mwenye nayo moja kati ya hizo ana sifa ya unafiki hadi aiache:

Anapoaminiwa anafanya *khiyaanah*,

---

Anapozungumza anazungumza uongo,
Anapoingia katika ahadi, anakhalifu,
Na anapoingia migogoro na watu wengine, anakuwa na tabia mbaya."

**[Hadiyth sahihi iliyopokewa na al-Bukhaariy na Muslim]**

**Mtu anayechanganya sifa hizi nne kwa hakika amechanganya uovu wote na sifa zote za unafiki. Lakini aliyekuwa nayo moja kati ya hizo, anakuwa na sifa ya unafiki. Mtu anaweza kuwa na sifa zote za uzuri na ubaya, na halikadhalika *Iymaan*, ukafiri, na unafiki – atastahiki kupewa malipo au adhabu kwa mujibu wa sifa ambazo zinastahikia kwa moja kati ya hizo, kama vile kuwa na uvivu kuhudhuria *Swalah* za *jamaa'ah* msikitini, kwa hili ni katika tabia za kinafiki. Unafiki ni uovu na ni hatari na Maswahaabah walikuwa wakihofia kuutumbukia. Ibn Abiy Mulaykah amesema: 'Nimekutana na Maswahaabah thelathini wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam), kila mmoja wao akihofia unafiki kwa nafsi yake."**

**-mwisho wa maneno ya Shaykh Al-Fawzaan-**

S2. Kufr ni kinyume cha *Iymaan*. Je, kila aina ya kufr inamtoa mtu nje ya Uislamu?

**Jibu: Hapana.**

**Katika namna sawa ambayo shirk na unafiki kila moja kuweza kuwa ni aina kuu au ndogo, kufr pia ni ya aina mbili: kuu na ndogo. Aina kuu ya *shirk/kufr/*unafiki ni aina ambayo inamtoa mtu nJe ya Uislamu. Aina ndogo ya *shirk/kufr/*unafiki haimtoi mtu nje ya Uislamu. Hii inaelezwa na Shaykh Swaalih al-Fawzaan ndani ya "Kitabu cha Tawhiyd/"Aqiydah Tawhiyd".**

***Haditzyh* ambazo ni sahihi, iliyotajwa na Imaam Ahmad nukta 70, inaweza kwa namna zote kufafanuliwa kuhusisha unafiki mdogo au ukafiri mdogo – aina ambazo hazimtoi mtu nje ya Uislamu. Hata hivyo, kuna makundi potofu ambayo yanaharibu maana ya *Hadiyth* hizi, na *Hadiyth* hizo ambazo zinafanana nazo, zinadai kwamba matendo yaliyotajwa yatamtoa mtu nje ya Uislamu moja kwa moja.**

S3. Kwa mujibu wa Imaam Ahmad, ni yepi yafuatayo tuyatende pale tutakapokutana na *Hadiyth* sahihi ambayo maelezo yake hatuyaelewi?

1. Kuikubali
2. Kuijadili
3. Kuikataa

**Jibu: 1 Angalia nukta 70 ya 'Misingi Ya Sunnah'.**

S4. Maelezo gani yafuatayo ni sahihi kuhusu Pepo na Moto?

1. Tayari zimeshaumbwa.
2. Zitaumbwa Siku ya Hukumu.
3. Hakuna anayefahamu iwapo tayari zimeumbwa au laa.

**Jibu: 1.**

**Kuna *Hadiyth* nyingi zinazothibitisha kwamba tayari zimeshaumbwa. Angalia 'Misingi Ya Sunnah' na hadidu za chini za baadhi yake.**

S5. Matamko gani yafuatayo ni sahihi kuhusu kuthibitisha kwamba Pepo na Moto ni kweli?

1. Ni lazima kuthibitisha kuwepo kwake.
2. Kuthibitisha kuwepo kwake ni jambo ambalo linawezekana kwa hoja na kwa mtu ambaye ameingizwa Peponi.
3. Kuna watu kutoka dhehebu la Jahmiyyah wanaokataa kwamba watu wataadhibiwa Motoni.

**Jibu: Zote hizo ni sahihi.**

**Ama kwa 1 na 2, Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) amesema:**

"Yeyote anayeshuhudia kwamba hakuna apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah pekee, asiyekuwa na mshirika, na kwamba Muhammad ni Mtumwa Wake na Mjumbe Wake na kwamba 'Iysa ni mtumwa wa Allaah na mjumbe Wake, (aliyeumbwa kupitia) Neno Lake ambalo Amelifikisha kwa

Maryam, na roho [iliyoumbwa] na Yeye na kwamba Moto ni Haki, Allaah atamuingiza Peponi kwa yale ambayo ameyatenda." **[Hadiyth sahihi iliyopokewa na al-Bukhaariy na Muslim]**

**Katika kitabu cha Al-Mulakhkhas (ufafanuzi wake wa Kitaabut Tawhiyd) cha Shaykh Swaalih al-Fawzaan kinaeleza kwamba Hadiyth hii inaonesha kwamba ni lazima kuamini kuhusu Pepo na Moto.**

**Katika kitabu cha Ufafanuzi wa *Iymaan* nukta 84, al-Barbhaariy anaeleza: "[Ni lazima] kuwa na *Iymaan* kwamba Allaah, Mtukufu na Mkubwa, ataadhibu vilivyoumbwa ndani ya Moto, kwa minyororo, vyuma na pingu. Moto utakuwa ndani yao, juu yao na chini yao. Ingawa, Jahmiyyah, miongoni mwao ni Hishaam al-Fuutiy amesema: 'Isipokuwa ni kwamba Allaah Atawaadhibu karibu na Moto.' Hii (tamko hili) ni kumkana Allaah na Mtume wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam)."**

Darasa hili ni fupi kuruhusu muda wa jaribio la mara moja kwenye kitabu chote.

-MWISHO-